SportPesa
TZS. 537,737,060
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Kifo** cha Ole Nasha chashtua wengi, dereva wake atoa neno

UKURASA 4



Ramsey kuwekwa sokoni Juve

UKURASA 23

Nipashe
Jumatano Septemba 29, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya
ISSN 0856 • Na. 0580718
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Hamasa chanjo ya corona moto

• **Rais** ahimiza viongozi wa dini, ujumbe wa mitandao simu wahamasisha, watumishi ardhi wachanjwa ofisini...*Endelea ukurasa 2 & 3*



Rais Samia Suluhu Hassan, akifungua kongamano la wachungaji na maaskofu wa Kanisa la Anglikana Tanzania na maadhimisho ya miaka 50 ya kanisa hilo, katika viwanja vya Chuo Kikuu cha St. John's, jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 2
**KUMRADHI**
KATIKA toleo letu la jana kwenye ukurasa wa kwanza tulichapisha habari yenye kichwa 'Samia akerwa na...

UKURASA WA 5
**MAREKANI YAADHIMISHA KUMBUKUMBU YA MIAKA 60 YA UWAPO WA PEACE CORPS NCHINI TANZANIA**

UKURASA WA 16
**WAHUKUMIWA KUNYONGWA HADI KUFA KWA MAUAJI**
MAHAKAMA Kuu ya Tanzania, Kanda ya Mbeya, imewahukumu kunyongwa hadi kufa watu wawili wakazi wa...

## Machinga watoa ya moyoni machungu bomoabomoa

UKURASA 3



KESI YA MBOWE

## Shahidi adai mwenzao hajulikani kama yu hai

UKURASA 2

MICHEZO AZAM YAJISAHAULISHA YA COASTAL UK.20
MAONI, KATUNI UK.6

# Hamasa chanjo corona yapamba moto

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HAMASA kwa ajili ya chanjo ya corona imezidi kupamba moto huku Rais Samia Suluhu Hassan, akiwahimiza viongozi wa dini kufanya kampeni ya kutosha ya kuhimiza wananchi kupata chanjo ya corona.

Sambamba na wito huo, amewataka viongozi hao kuhamasisha waumini wao kushiriki kwenye sensa ya watu na makazi itakayofanyika mwakani.

Wakati Rais akitoa hamasa hiyo kwa viongozi wa dini ambao wana mtandao wa waumini wengi, pia mitandao ya mawasiliano imeshinikiza suala hilo kwa kutuma ujumbe mfupi kwa njia ya simu.

Samia aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza kwenye maadhimisho ya miaka 50 na kongamano la wachungaji na maaskofu wa Kanisa la Anglikana Tanzania.

"Niwaombe viongozi wa dini kujumuisha masuala ya sensa kwenye mahubiri yenu ambayo itaanza mwakani. Tumeanza kwa majaribio maeneo mbalimbali, sasa wahimizeni waumini wakubali kuhesabiwa.

"Serikali ikitoa masuala ya sera ina shughuli nyingi, anatokea tu kiongozi wa dini kupinga na bado maamrisho yake kwenye kitabu chake hayamtumi hivyo kwa hiyo naomba sana nendeni kuhimiza suala la sensa," alisema.

Aliwaomba kupiga kampeni ya kutosha kwenye suala la corona kwa kuwa chanjo inapunguza vifo na makali ya maumivu ya ugonjwa huo.

"Tuwaelimishe waumini wetu wakubali kuchanjwa. Si, lazima wengine wanasema si lazima ila hajui akichanja anapata nini na asipochanja anapata nini, hivyo naomba mtusaidie kuwaelimisha lakini chanjo ni kinga tu na kwa bahati nzuri wakati natembelea maonyesho hapa vijana wa kanisa hili wamenionyesha kazi yao wanazalisha wanatengeneza kinga.

"Wakitengeneza na kuingiza kwenye majimaji itakuwa chanjo. Kwa hiyo ni chanjo tu kama hawataamini inayotengenezwa na watu wetu ikikamilika na kugeuzwa kuwa maji ikitoka kwenye sindano na ipigwe mtu anaamini kwa sababu imetengenezwa hapa," alisema.

Rais aliwapa moyo vijana wanaotengeneza kinga hiyo kutengeneza kwa wingi ili ipelekwe kwenye taasisi za kimataifa za afya ziangaliwe na wananchi wachanjwe hizo.

"Kama zitakubaliwa watu wetu wachanje hizo kwa sababu chanjo ni kinga tu. Wazungu walifanya kinga kwa vitu vyao walivyotumia na hapa tunafanya kinga kwa vitu tunavyotumia, lakini vitu vingine ni miti tu ambayo vijana wetu wa Anglikana wameitumia," alisema.

Alisisitiza kuwa chanjo ni kinga inayotokana na miti na kuwapongeza vijana hao kwa hatua hiyo na serikali itawasaidia kufika taasisi za kimataifa ili watambulike.

**HAMASA MTANDAONI**

Wakati Rais Samia akiagiza hivyo, hamasa kuhusu wananchi kujitokeza kupata chanjo hiyo imezidi kupamba moto baada ya ujumbe kusambaa kuwataka watu kuchanja ili kujiepusha na maradhi ikiwamo corona.

"Chanjo ya corona itakukinga na ugonjwa, kulazwa na hatari ya kifo. Fanya uamuzi wa kupata chanjo. Wahi sasa," ulisomeka ujumbe mfupi wa maandishi kwa njia ya simu (sms).

**RAIS APONGEZA**

Awali, alisema taasisi za dini zina mchango mkubwa katika kudumisha amani na kujenga umoja wa taifa.

Kanisa hilo lina vituo 40 kutolea huduma za afya 40, hospitali saba na taasisi 63 za elimu, hivyo akalishukuru kwa kutoa huduma hiyo kwa Watanzania bila kujali dini, rangi wala itikadi za kisiasa.

Kutokana na huduma hizo, alisema serikali itaendelea kuwapa ushirikiano wa kutosha ikiwamo kuendelea kuwapatia mikopo ya elimu ya juu wanafunzi wa vyuo vikuu vinavyomilikiwa na kanisa na kutoa vifaa tiba, vitendanishi, kuajiri na kulipa mishahara kwa watumishi wa afya kwenye hospitali zinazoendeshwa kwa ushirikiano na serikali.



Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Prof. Faustine Bee (kushoto) na Ofisa Mkuu wa Biashara wa Benki ya CRDB, Dk. Joseph Witts, wakitia saini mkataba wa makubaliano ya ujenzi wa geti kuu la kisasa katika chuo hicho, jijini Dodoma jana, ambapo benki hiyo italijenga kwa gharama ya Sh. milioni 150. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shahidi kesi ya Mbowe adai hawajui mwenzao kama yu hai

**Na Kulwa Mzee**

MSHTAKIWA wa tatu katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na wenzake watatu, Mohammed Ling'wenya, amedai ushahidi wa Inspekta Mahita Omary ni wa uongo.

Alidai Mahita aliyedai kuwa walikuwa wakimtafuta Moses Lijenje bila mafanikio sio kweli, walikuwa naye Lau Madukani, Moshi lakini hadi leo hajui kama yuko hai ama amekufa.

Hayo yalibainika jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, mbele ya Jaji Mustapha Siyani, wakati Ling'wenya akiongozwa na Wakili wa utetezi Nashon Nkungu kutoa ushahidi.

Ling'wenya ambaye ni shahidi wa pili katika shauri dogo, alidai alikuwa na Adamu Kasekwa na Moses Lijenje, Lau Madukani na wote walikuwa wanatarajia kupata ajira ya ulinzi kwa Mbowe, lakini Moses hajawahi kumuona mpaka leo.

Alidai Moses alikuwa Kikosi cha 92 KJ kabla yake na kwamba akiwa Kituo cha Polisi Tazara wakitaka kuelekea Mbweni, afande Goodluck alimwambia atamtupa kama Lijenje, maneno ambayo yalimtisha kwa sababu anajua kutupa ni kuuawa au kutupwa Mto Wami bila kuzikwa.

"Nilipata hofu sababu Lijenje tulikuwa naye Madukani na sijamuona hadi leo.

Akihojiwa na Kibatala alidai mpaka leo hafahamu kitu kuhusu Lijenje, anaweza kuwa amekufa ama yuko hai.

Pia, alidai Moses alikuwa Kikosi 92 KJ kabla yake na hajawahi kusikia kama alishtakiwa na wala hajasikia kama atakuja kuunganishwa kama mshtakiwa.

Kadhalika alidai ushahidi uliotolewa na Inspekta Mahita Omary kwamba walikaa muda mrefu Moshi wanamtafuta Moses sio wa kweli.

Aliendelea kudai kuwa alifikishwa Kituo cha Polisi Mbweni Agosti 9, 2020 na akiwa mahabusu hajawahi kupelekewa ndoo ya chakula kama mahabusu wengine hadi alipofikishwa mahakamani Agosti 19, 2020 ndipo alipopewa wali dagaa.

"Nilikaa siku kumi bila kupewa chakula na waliotakiwa kufanya hivyo kisheria, koplo mmoja ndiyo alikuwa akiingia zamu ananiletea soda, biskuti au maji, huyo ndiyo nilikuwa namtuma kwa Kasekwa," alidai Ling'wenya.

Akihojiwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Abdallah Chavula, shahidi alidai alikula kiapo kulitumikia jeshi hadi mwisho, kulinda amani ya nchi na vifaa vya kijeshi.

Alidai kuwa alikuwa mwalimu wa Makomandoo, mshtakiwa Kasekwa ni mwanafunzi wake na wapo wengine wengi ambao wanafika gerezani kumuona.

"Nimepigana vita Kongo, nilipata mafunzo ya kupigana kareti, kick box, kuzuia maharamia waliokuwa wanafanya magendo baharini, nilifundishwa na Wafaransa jinsi ya kuwakabili kwenye maji.

"Nilifundishwa kupigana kwenye majumba, nilijifunza jinsi ya kuwatoa maadui kwenye nyumba, nilijifunza kutumia SMG na kisu," alidai.

Kutokana na mafunzo aliyopata, alidai anaweza kukabiliana na adui mahali popote, lakini hawezi kujua komandoo mmoja anaweza kukabiliana na askari wengine wangapi.

"Askari wasiokuwa na mafunzo labda wawili, watatu naweza kuwakabili."

"Baada ya mazungumzo kesho yake Lijenje alitupigia simu, tulimwambia tulipo akatufuata Madukani, alikaa baa, mimi nilikuwa dukani na Kasekwa alikuwa anaongea na simu akavamiwa na kupigwa.

"Katika tukio lote Lijenje sikumuona, sijui alikuwa wapi," alidai Ling'wenya ambaye alifunga ushahidi wake.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Halfani Bwire, Adam Kasekwa na Mohammed Ling'wenya ambao wote wanakabiliwa na mashtaka sita yakiwamo ya kula njama kufanya vitendo vya ugaidi.

Kesi iliahirishwa hadi leo kwa ajili ya shahidi wa tatu katika kesi ndogo.

## KUMRADHI

KATIKA toleo letu la jana kwenye ukurasa wa kwanza tulichapisha habari yenye kichwa 'Samia akerwa na chanjo ya corona majumbani'.

Hata hivyo, kichwa hicho cha habari hakikuakisi maudhui yaliyokuwa katika habari hiyo, kwa kuwa alichokieleza Rais Samia juzi jijini Dodoma kwenye ufunguzi wa Mkutano Maalum wa Uchaguzi wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT) ni kuwataka wataalamu wa afya nchini kutoa elimu kwa wananchi, ili wahamasike kuchanja chanjo ya Uviko-19.

Rais Samia hakutamka neno 'kukerwa' bali alisema badala yake wataalamu waendelee kutoa elimu kwa kutumia njia wanayotumia sasa ya kutembea nyumba kwa nyumba kuchanja watu.

"Mtaalamu unaweza kwenda katika nyumba na kumwambia mtu unataka kuchanja akasema sitaki ukaondoka, lakini kumbe kama elimu ingetolewa ya kutosha basi hili jambo lingekuwa jepesi sana."

Aliwataka wataalamu wa afya kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi ili kuwahamasisha kuchanja kwa hiari yao bila kutumia mabavu.

"Tuandae kampeni kabambe ambayo itasaidia kufikisha elimu kwa wananchi wetu ili watambue umuhimu wa kupata chanjo ya Uviko-19 na kupunguza vifo vitokanavyo na janga hili," alisema Rais Samia.

Kadhalika, alisema hivi sasa wananchi wanaonekana kuwa wagumu kupata chanjo kutokana na kutopatiwa elimu ya kutosha kuhusu umuhimu wa chanjo hiyo.

"Kuna mtu anaweza kuwa mgumu kupata chanjo kwa sababu hajapata ile adha ambayo wengine wameipata kama kuondokewa na ndugu yake wa karibu au mjomba wake, akaona namna ambavyo ugonjwa huu ulivyo hatari, njia pekee ya kuwakomboa hawa ni kuwapatia elimu ya kutosha," alisisitiza.

Tunamwomba radhi Rais Samia na Watanzania kwa ujumla kwa usumbufu wowote uliojitokeza.

**Mhariri**




Mkurugenzi Mtendaji wa Airtel Money, Isaac Nchunda (kushoto), akizungumza jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa huduma ya mkopo kwa kupitia simu za mkononi inayoitwa "KAMILISHA" kwa ubia na Benki ya I&M. Kulia ni Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dk. Bernard Kibesse. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Watumishi Wizara Ardhi wachanjwa corona ofisini

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

WATUMISHI wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, wameanza kupata chanjo ya corona katika ofisi za wizara zilizoko Mtumba katika mji wa serikali mkoani hapa.

Wataalamu wa afya kutoka Jiji la Dodoma wakiongozwa na Mganga Mkuu wa Jiji, Dk. Revocatus Kitena ndio walioendesha kuchanja watumishi hao ikiwa ni jitihada za kuhamasisha watumishi kuchanja ili kujikinga na corona.

Akizungumza wakati wa kazi hiyo, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Zakariya Kerra, alisema mchakato huo utafanyika kwenye ofisi zote za makao makuu ya wizara na zingine kwa wale watumishi ambao hawakupata chanjo.

"Watumishi wote ambao hawakupata chanjo sasa wanaweza kupata kupitia wataalamu wa afya wa Jiji la Dodoma wanaotembelea ofisi yetu na watafanya kazi hiyo kwa siku tatu kuanzia leo (jana) hadi Septemba 30," alisema.

Mkurugenzi huyo aliwataka watumishi wa wizara kwenye ofisi ambazo haziko kwenye mji wa serikali wa Mtumba kuwa tayari kupata chanjo hiyo kupitia ofisi zao.

Kerra alizitaja ofisi zingine za wizara kwa mkoa wa Dodoma ambazo haziko kwenye mji wa serikali Mtumba kuwa ni zile za uhasibu zilizoko Dodoma mjini, Upimaji, Maendeleo ya Makazi na Uthamini zilizoko Nanenane pamoja na Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani na kusisitiza watumishi wake wanatakiwa kukaa tayari kupata chanjo hiyo.

Serikali imewataka wataalamu wa sekta ya afya kuanza kuhamasisha wananchi wakiwamo watumishi wa umma kwa kuwafuata ofisini kwa ajili ya kupata chanjo ya Uviko-19, ili kujikinga na ugonjwa wa corona ambao umechukua uhai wa watu wengi duniani.

# Machinga waeleza machungu ya bomoabomoa

**Na Maulid Mmbaga**

KAZI ya kubomoa vibanda vya wafanyabiashara wadogo 'machinga' katika maeneo yasiyo rasmi mkoani Dar es Salaam imeleta kilio kwao, huku wakisema imewadidimiza kiuchumi na kurudisha nyuma maendeleo yao.

Mwishoni mwa wiki baada ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, kuzindua rasmi mpango wa kuwapanga wafanyabiashara, alfajiri ya Septemba 23, mwaka huu machinga katika eneo la Gongo la Mboto walilalamika kuvunjiwa vibanda vyao, huku wengine wakidai kupoteza baadhi ya bidhaa zao.

Wakizungumza na Nipashe, walieleza kuwa kubomolewa vibanda vyao kumewarudisha nyuma kimaendeleo, kwani walikuwa wanajikimu kimaisha kupitia biashara hizo.

Maimuna Iddy, alieleza kuwa wanafanya biashara kwa kuwafuata wateja walipo, huku akidai kuwa maeneo wanapoelekezwa kwenda kuna changamoto ya kufanya biashara kutokana na mzunguko wa watu kuwa mdogo.

Pia, alidai kwamba kwa asilimia kubwa wanategemea kipato kinachotokana na biashara ndogo ambayo ndiyo inayomsaidia kukidhi mahitaji ya kila siku kama kulisha familia, kusomesha watoto na kulipa kodi mbalimbali za serikali.

"Kitendo cha kubomolewa vibanda na kuondolewa sehemu tunazofanyia biashara kinachangia kutudidimiza kiuchumi na kimaendeleo, hivyo tunaiomba serikali kupitia manispaa itujengee vibanda kwa mpangilio wanaoupendekeza wenyewe, watupangishe tuwe tunawalipa kodi ili watuache tuendelee na biashara.

"Siyo kwamba tunapinga maelekezo ya serikali ila huku tulipokuwa ndipo wateja walipo, tukiondoka na kwenda mbali ni vigumu kutufuata na ili maisha yaendelee ni lazima tufanye biashara ili kumudu gharama za maisha," alisema.

Saidi Liaheja, anayejishuhulisha na uuzaji wa nguo za mtumba alisema uamuzi wa uongozi wa mkoa kuchukua hatua ya kuvunja vibanda vyao vya biashara si wa kiuungwana na umewapa hasara kwani walitumia gharama katika kuviandaa.

Alisema wakati uvunjaji wa vibanda ukiendelea, kuna baadhi yao waliacha vitu vyao ikiwamo meza ambazo nazo walizikuta zimeharibika jambo ambalo kwa upande wao halikuwa na tafsiri nzuri.

Wakati hayo yakiendelea tayari manispaa zote ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam zilishaweka mabango ya matangazo yenye katazo la kufanya biashara kwenye hifadhi za barabara.




# Kifo cha Ole Nasha chashtua wengi, dereva wake atoa neno

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

KIFO cha Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, William Ole Nasha, kimewashtua wengi huku dereva wake akidai kuwa hakuwa na dalili za kuzidiwa na ugonjwa wowote.

Akizungumza na Nipashe jana, Fikiri Madinda ambaye ni dereva wa Ole Nasha, aibainisha kuwa juzi walikuwa safarini kutoka Arusha kikazi ambapo walianza safari saa tano asubuhi na kufika Dodoma saa 10 jioni.

"Jana (juzi) nilipofika kumchukua hotelini alinijulisha kuwa usiku wa kuamkia hiyo jana (juzi) alisumbuliwa na presha lakini akaniambia kuwa kwa muda huo yuko sawa, hivyo tuanze safari," alisema Madinda.

"Tangu tuondoke Arusha hakupata tatizo lolote njiani hadi tulipofika nyumbani kwake eneo la Medeli na kuagana naye kuwa nimfuate leo (jana) saa 3:00 asubuhi kumpeleka ofisini," aliongeza.

"Lakini leo (jana) nimesikitika sana nilipopata taarifa kwenye mitandao za kifo chake. Imenisumbua sana kwa sababu ni mtu tuliyeachana naye na hakuonyesha dalili za kuzidiwa na ugonjwa wowote," alisisitiza.

**SAMIA,CCM WAMLILIA**

Rais Samia Suluhu Hassan, alisema Ole Nasha alikuwa mchapakazi na hodari katika sekta aliyokuwa na mtumishi mwaminifu kwa serikali na ametoa mchango mkubwa katika ujenzi wa taifa.

"Nasikitika kuwajulisha kuwa aliyekuwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwezeshaji, William tate Ole Nasha, amefariki dunia jijini Dodoma. Natoa pole kwa Spika Mhe. Job Ndugai, wabunge, familia na wananchi wa Ngorongoro. Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Amina,' aliandika Rais Samia katika ukurasa wake wa Twitter. Pia Taarifa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kupitia kwa Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, ilisema chama hicho kimepokea kwa mshtuko kifo cha Naibu Waziri huyo na kueleza kuwa alikuwa kiongozi mwaminifu na mzalendo ambaye wakati wote alijituma kwa bidii na juhudi kubwa katika ujenzi wa nchi.

"Chama na Serikali kimempoteza kiongozi mahiri, msikivu, hodari na aliyekuwa tayari muda wote kutekeleza mjukumu yake kwa ufanisi na weledi. Aidha, alitumia muda wake mwingi katika kuwatumikia wananchi na taifa kwa ujumla," alisema Shaka katika taarifa hiyo.

Pia alisema Ole Nasha alihudumu katika nafasi mbalimbali ndani ya chama na serikali ikiwamo mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa wa Arusha, Naibu Waziri katika wizara mbalimbali hadi umauti unamfika.

**BUNGE NA WABUNGE**

Katika ya Bunge, Spika Job Ndugai alisema amepokea kwa masikitiko taarifa za kifo hicho ambaye alikuwa Mbunge wa Ngorongoro na kwamba Ofisi ya Bunge inafanya mawasiliano na serikali kuhusu taratibu za mazishi na taarifa zaidi zitatolewa.

Naye Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, alisema Ole Nasha alikuwa mtu mwema, mstaarabu, mpole na rafiki wa kila mtu.

Mbunge wa Maswa Mashariki, Stanslaus Nyongo, alisema alikuwa kiongozi mwema na asiye na makuu na mtu.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana na wenye Ulemavu, Jenista Mhagama (wa pili kushoto), akikabidhi zawadi kwa Mkurugezi Mtendaji wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Dk. Aggrey Mlimuka, iliyotolewa na chama hicho wakati wa hafla ya kumpongeza na kumuaga baada ya kumaliza muda wake wa utumishi, jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi wa Chama hicho, Jayne Nyimbo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Auawa kwa madai ya kumroga baba mkwe

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MWANAMKE Limi Kulwa (30) mkazi wa kijiji cha Ilunga wilayani Kahama mkoani Shinyanga, ameuawa kwa kukatwa mapanga kwa tuhuma za kumroga baba mkwe wake, Lusana Kulwa (60).

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, George Kyando, alibainisha hayo jana, kuwa tukio hilo lilitokea juzi saa 4:30 usiku nyumbani kwa mwanamke huyo.

Alisema mwanamke huyo anadaiwa kuuawa na mdogo wa kaka yake, ambaye hakutaka kumtaja jina kwa sababu za kiupelelezi, kuwa alimkata mapanga kichwani, usoni na mikono yote na kusababisha kifo chake.

"Mtuhumiwa baada ya kutekeleza mauaji haya alikimbilia kusikojulikana, wakati wa utekelezaji wa mauaji, alimvamia marehemu wakati akipika jikoni, na kuanza kumkata mapanga bila mumewe kuwapo nyumbani," alisema Kyando.

"Chanzo cha mauaji haya ni marehemu kutuhumiwa kumroga baba mkwe wake, ambaye alifariki dunia Julai kwa maradhi," aliongeza.

Kyando alisema Jeshi la Polisi linawashikilia watu sita wa familia ya mumewe kwa mahojiano zaidi pamoja na kumsaka mtuhumiwa wa mauaji hayo.

Aliwaonya wananchi mkoani Shinyanga kuacha kujihusisha na imani potofu za kishirikina na kuwaua watu wasio na hatia.

# Rais ataka tathmini kodi huduma elimu, afya kwa taasisi za dini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ameagiza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kufanya tathmini ya kodi kwa taasisi za dini zinazotoa huduma za elimu na afya.

Akizungumza jana jijini hapa kwenye maadhimisho ya miaka 50 na kongamano la wachungaji na maaskofu wa Kanisa la Anglikana Tanzania, Rais aliagiza kodi hizo ziangaliwe vizuri ili kufahamu zipi zinatoa huduma na zipi zinafanya biashara.

"Kuhusu kodi niliagiza kwa zile taasisi za dini zinazotoa huduma ya elimu na afya si zinazofanya biashara ya elimu na afya lakini huduma ya elimu na afya kodi ziangaliwe kwa sababu tumeliangalia suala hili malalamiko yalikuja siku nyingi. Tunaliangalia tukakuta viwango vinavyotozwa kwenye taasisi za dini vya afya na elimu havipishani viwango na wanaotoa huduma sekta binafsi.

"Sasa wale wa sekta binafsi wanafanya faida bila shaka na kama viwango ni vile kwa taasisi za dini wanapata faida bila shaka, sasa haka kafaida haka basi kachangie kwenye serikali pia. Kwa zile zinazotoa huduma tutaangalia suala la kodi lakini kwa zile zinazofanya biashara lazima biashara ichangie kodi kwenye serikali," alisema.

Awali, Askofu Mkuu wa Kanisa hilo, Dk. Maimbo Mndolwa, aliomba serikali iboreshe mfumo wa utoaji wa vibali vya huduma mbalimbali ikiwamo vya kuanzisha dayosisi.

"Kuna changamoto ya kanisa kutakiwa kulipa kodi kiasi zinazotishia kufunga baadhi ya huduma zetu ambazo tunafanya kama ibada, kwa mfano shule na hospitali mbalimbali za kanisa. Pamoja na kutoa huduma kwa jamii zinatakiwa kulipa kodi ya ardhi na kodi zingine ambazo haziendani na mapato ya hospitali na shule hizo.

"Tunashukuru masuala ya kodi kwenye taasisi za dini tayari serikali yako kwa kujali sana mahusiano yaliyopo inaangalia vyema mambo hayo, lakini iyaangalie kwa jicho la huruma kwa kuwa inasababisha baadhi ya taasisi hizi kutumia nguvu sana kujiendesha," alisema.

Akizungumzia masuala ya wanawake, alibainisha wanawake waliopo nchini ni zaidi ya asilimia 50 na hawapaswi kuachwa nyuma kwenye suala la maendeleo.

"Mkituacha nyuma sisi wanawake nchi itaendelea lini? Na malengo ya kimataifa yanatuambia hakuna mtu ambaye aachwe nyuma kwenye kwenda na maendeleo. Sasa mnavyodondosha wanawake mkawanyima haki zao, mkawaonea kwenye mirathi, kunyang'anya ardhi yao maendeleo yatakuja lini?"

"Nguvu ya kanisa isiwe kuwafanya wanawake wakope. Isiwe kulea tu yatima lakini pia kujenga heshima ya wanawake wa Tanzania. Kanisa liseme kwa sauti kubwa kwenye hili. Tumezaliwa sawa na hata darasani tulikuwa tunawapita hata matokeo ya sasa yanaonyesha wanaongoza ni kina nani. Sasa inapokuja kwenye madaraka mnasema hafai, naomba mniunge nguvu kwenye hilo," alisema.

"Tunafanya hivyo si kwa sababu Rais ni mwanamke pia. La hasha! Tunafanya kwa sababu kwanza mwanamke ni kiumbe mwenye haki sawa na wengine anayezaliwa na mwanadamu.

"Tunapozaliwa ndugu zangu wote tunatoka sawa. Kuna mwanaume anakuja na kibaka hapa kuonyesha ana akili zaidi, kuna 'shape' ya kichwa inayoonyesha huyu ana akili zaidi, kuna mwanaume kazaliwa na nguo zake? Wote tunazaliwa sawa kinachotutofautisha ni makuzi na imani," alisisitiza.

Alisema mwanamke ana haki sawa na mwanaume kwenye jamii isipokuwa haki za kimungu kama vile kubeba mimba.

"Unaponiona mimi ni 'second citizen' ni mtu wa daraja la pili sikuelewi nami nitasimama na hilo, kuwanyanyua wenzangu twende pamoja," alisema.

# TANGAZO

**Ujumbe kutoka kwa Dkt. Donald Wright, Balozi wa Marekani nchini Tanzania**
**Kwa heshima ya maadhimisho ya miaka 60 ya Shirika la Huduma za Kujitolea za Wamarekani Peace Corps Tanzania**



Dr.Donald Wright
US Ambassador to Tanzania

Mwaka huu ni mwaka wa kipekee katika historia ya urafiki baina ya nchi ya Marekani na Tanzania. Tunasherekea maadhimisho matatu ambayo yametupata mafanikio makubwa katika nchi zetu zote. Adhimisho la kwanza ni kuhusu miaka 60 ya uhuru wa Tanzania. Adhimisho la pili ni kuhusu kuanzishwa kwa mahusiano ya nchi hizi mbili. Adhimisho la tatu ni lile la kumbukumbu ya miaka 60 ya uwepo wa Peace Corps hapa Tanzania.

Rais wa Marekani John F. Kennedy alianzisha Peace Corps mwaka 1961, kwa kuwapa changamoto vijana wa Kimarekani kwenda kuhudumu kwa kufanya kazi za ubinadamu kuleta amani na maendeleo katika nchi mbalimbali duniani. Kwa sababu ya urafiki wa karibu kati ya Rais Kennedy na muaasisi wa taifa la Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Tanzania (kwa wakati huo Tanganyika) ilichaguliwa kuwa nchi ya kwanza duniani kupokea Mavolontia wa Peace Corps. Mnamo tarehe 29, mwezi wa Septemba mwaka 1961 Mavolontia 50 wa Peace Corps walitua mjini Arusha.









Tangia hapo, takriban Mavolontia 3, 200 wa Peace Corps wamefanya kazi katika mikoa 22 ya hapa Tanzania kuboresha maendeleo katika jamii na kuchangiaa katika mchakato wa kufikia suluhisho la changamoto za elimu, afya na kilimo. Kwa mfano, mwaka 2019, kabla ya kuondolewa Mavolontia wa Peace Corps kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO -19, Mavolontia107 walifanya kazi kama walimu wa Sayansi, Tecknolojia, Uhandisi na Hisabati na masomo mengine ya sayansi,ambapo waliweza kufikia wanafunzi wapatao 13,000. Mavolontia sitini walifanya kazi kusaidia katika kilimo ugani na wengine sitini walifanyakazi katika sekta ya afya ya jamii. Matokeo yake, Mavolontia wa Peace Corps waliweza kufikia watu zaidi ya 6,000 katika mafunzo ya maji salama na usafi; zaidi ya watu 2,000 walipokea mafunzo ya elimu ya mama na mtoto na elimu ya malezi ya mtoto; watu 2,000 walipokea mafunzo ya kuzuia maambukizo ya VVU/UKIMWI; na zaidi ya watu,3,000 walipokea jumbe za kujikinga na kuzuia malaria. Pia, Mavolontia walifanya kazi na zaidi ya wakulima 1,000 na walisaidia vijiji 300 katika ufugaji.

Peace Corps ina athari chanya katika kizazi cha Watanzania na Wamarekani. Watanzania wengi ambao ni maarufu wanazungumzia vizuri sana mwigiliano wao na Mavolontia wa Peace Corps.Waziri wa mambo ya nje Liberata Mulamula mara nyingi amekuwa anasimulia ni kwa jinsi gani alikuwa akitiwa moyo alipokuwa anasoma na mwalimu wake ambaye alikuwa ni Volontia wa Peace Corps katika shule yake. Kwa kuongezea, Profesa Palamagamba Kabudi, Waziri wa Katiba na Sheria, na Profesa Sospeter Muhongo, aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini, wao pia walikuwa na uzoefu chanya na Mavolontia wa Peace Corps. Na kwa wakati huo huo, Mavolontia wa Kimarekani wa Peace Corps wana faida zilizo sawa katika uzoefu wao. Balozi Johnny Carson alikuwa Volontia wa Peace Corps hapa Tanzania toka mwaka 1965-1968. Alienda kuwa Balozi wa Marekani katika nchi za Kenya, Zimbabwe, na Uganda na alikuwa Naibu Katibu Mkuu wa serikali ya Marekani kwenye bara la Afrika.







Bila shaka, baadhi ya Mavolontia wa Peace Corps wametokea kuipenda Tanzania na kubaki kuwa wakazi na wajasiliamali. Peace Corps imekuwa ni daraja muhimu la kuimarisha uhusiano wa raia wa mataifa yetu haya.

Huko Marekani, Mavolontia wa Peace Corps waliowahi kuhudumu hapa Tanzania, wanazungumzia Tanzania ni nchi yenye utajiri wa utamaduni, historia na uzuri kwa Wamarekani. Vilevile, Watanzania wengi wamepata uelewa mzuri kuhusu Marekani kwa kuwa wamewakaribisha Mavolontia wa Peace Corps majumbani mwao; kula chakula pamoja,wakibadilishana mawazo na kuuenzi urafiki.

Hakuna Volontia wa Peace Corps anayefanya kazi peke yake, na bila msaada wa watanzania ambao hujitolea kukaa nao wakati wa mafunzo, wanakijiji, wafanyakazi wenza, na wafanyakazi wengine ambao wanashirikiana nao katika mazingira ya kazi zao na bila kuwasahau wafanyakazi hodari wa Peace Corps. Mavolontia wasingaliweza kutoa kazi nzuri iliyostawi na kuchangia maendeleo yao ya jamii zao. Na hii ndiyo sababu ninataka kuchukua nafasi katika hili tukio kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote ambao kwa namna moja au nyingine wamesaidia programu hii kwa muda wa miaka mingi. Ninapenda kuishukuru serikali ya Tanzania kwa msaada na ushirikiano na Peace Corps. Tunapoangalia mbele na kutazama nini ni mwelekeo wa baadaye wa programu ya Peace Corps hapa Tanzania, ninapata matumaini makubwa sana. Tunapanga kuwarudisha Mavolontia wa Peace Corps upesi iwezekanavyo ili waendelee na kazi nzuri waliyokuwa wanaifanya. Peace Corps inatumaini Tanzania itaendelea kuwakaribisha Mavolontia katika jamii zao.

Maadhimisho haya ya miaka 60 ya uhusiano wetu mzuri hutumika kama hatua muhimu katika ushirikiano kati ya serikali hizi na watu wa Marekani na Tanzania. Tunatumaini mtashikiana nasi katika kusherekea maadhimisho ya miaka 60 ya ( Peace Corps) Tanzania. Pamoja!





Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kalamu ya Samia iwafute wasiotekeleza wajibu wao

**VIONGOZI** wa kuteuliwa katika ngazi za wilaya na halmashauri wamepewa angalizo, kutokana na kuendeleza malumbano na kutokuelewana, hivyo kutowahudumia wananchi.

Hao ni wakurugenzi wa halmashauri, wakuu wa wilaya na makatibu tawala wa wilaya, ambao wajibu wao ni kusimamia shughuli za maendeleo pamoja na kuwatatulia wananchi vikwazo na kero zinazowakabili.

Kwa kuliona tatizo hilo, Rais Samia Suluhu Hassan, ameeleza kukerwa na ugomvi kwa watumishi wa umma wakiwamo wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri na kuahidi kuwa hatozungumza kitu bali kalamu yake ndiyo itakayozungumza.

Alitoa kauli hiyo juzi jijini Dodoma wakati wa ufunguzi wa mkutano mkuu maalum wa uchaguzi wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), na kwamba amekuwa akishangazwa na namna ambavyo viongozi wa umma aliowateua kwenda kumwakilisha wakiacha majukumu yao na kufanya mambo yenye maslahi yao binafsi.

Alisema uongozi wa juu unawaona wanavyolumbana badala ya kutatua kero za wananchi ambazo ndizo zimewaweka katika nafasi walizonazo sasa.

Aidha, alisema kutokana na ugomvi huo maeneo hayo yamekosa maendeleo na kuwafanya wananchi kuendelea kupata shida ya huduma mbalimbali za jamii ikiwamo afya, elimu na miundombinu ya barabara.

Kauli ya Rais Samia kuhusu utendaji usioridhisha wa viongozi wengi ngazi ya wilaya ni mwendelezo wa kauli zilizowahi kutolewa na viongozi wakuu wa nchi waliomtangulia.

Hali hiyo ndiyo imekuwa ikisababisha wananchi kuvamia misafara ya viongozi wakuu wa taifa wanapokwenda vijijini wakati mwingine wakiwa wamebeba mabango yaliyoandikwa maneno kuhusu kero zinazowakabili.

Kwa kuamua kufanya hivyo, tafsiri yake ni kwamba viongozi walioko kwenye maeneo hayo hawaendi kwa wananchi kusikiliza matatizo yao na kuyatafutia ufumbuzi. Huo sio uwajibikaji.

Haiwezekani Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu waende wilaya zote nchini kwa ajili ya kusikiliza kero za wananchi na kuzipatia ufumbuzi, hivyo ndiyo maana kukawapo na wawakilishi wao kuanzia mikoa hadi wilaya kwa ajili ya kutekeleza majukumu hayo.

Rais alisema maslahi binafsi ndicho chanzo cha migongano baina ya viongozi hao ya kutaka kutumia vibaya fedha za maendeleo zinazotumwa na serikali katika halmashauri husika.

Viongozi wa aina hiyo waliokula kiapo cha maadili hawapaswi kuwapo katika utumishi wa umma, kwa sababu wanaiharibu taswira ya serikali kwa wananchi, hivyo suluhisho ni kuwaondoa na kuweka wanaoweza kutanguliza maslahi ya umma.


Tunakubaliana na alichokisema Rais Samia kwa kuwa ndicho kinachoshuhudiwa katika maeneo kadhaa nchini, kutokana na wananchi kukimbilia kutoa kero zao za maji, afya, elimu, barabara, ardhi na mambo mengine madogo ambayo yanaweza kutatuliwa na viongozi wao.

Tunaona njia pekee ya kuwafanya viongozi wawajibike kwa utumishi wa wananchi ni kuwapangia malengo ambayo ni kuzisikiliza kero na kuzipatia ufumbuzi kwa wakati mwafaka.

Wale ambao wataendeleza malumbano na kufanyakazi kwa mazoea bila kuleta matokeo, ni sahihi Rais Samia atumie kalamu yake kuwafuta kazi badala ya kuwapigia kelele na kuwafokea kila wakati kuwakumbusha wajibu wao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Watu wanasubiri asilimia 40 ya mapato kusisimua maendeleo

Na Reubeni Lumbagala

**KASI** ya maendeleo ya nchi na ustawi wa maisha ya raia unategemea utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayogusa maisha yao.

Uibuaji na utekelezaji wa miradi hiyo unategemea kupatikana, kutenga na matumizi bora ya fedha zinazoonyesha thamani halisi ya pesa kwenye kile kilichofanyika.

Katika kutekeleza miradi ya maendeleo ya wananchi, ushirikiano wa serikali kuu pamoja na za mitaa au halmashauri za wilaya ni muhimu ili kupata fedha na kuzitumia kiusahihi.

Hivyo basi, serikali za mitaa kupitia halmashauri za wilaya, zina wajibu wa kuhakikisha zinashiriki kikamilifu katika kutenga asilimia 40 ya mapato ya ndani ili fedha hizo zitumike kukamilisha miradi ambayo inagusa maisha na ustawi wa wananchi pamoja na kuongeza vyanzo vya mapato kupitia miradi hiyo ya maendeleo iliyoibuliwa.

Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) imetoa mapendekezo na maagizo ikiwataka wakurugenzi wa halmashauri kutenga asilimia 40 ya mapato ya ndani kwa ajili ya kukamilisha miradi hiyo.

Aidha, inapendekeza Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuzisimamia halmashauri kikamilifu ili zitenge asilimia 40 ya mapato yake, kama zinavyoagizwa.

Ikumbukwe kuwa kutenga mapato hayo si hisani za wakurugenzi bali ni kisheria. Lakini kumekuwa na kusuasua kwa baadhi ya halmashauri kutekeleza takwa hilo na kuathiri miradi ya maendeleo katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Kushindwa kutengwa kwa asilimia 40, kunazorotesha kuibua, kutekeleza miradi hivyo kurudisha nyuma jitihada za kukatua kero za wananchi na kurudisha nyuma kasi ya maendeleo.

Miradi ya maendeleo kama vile ujenzi wa vituo vya afya, masoko, vituo vya mabasi, shule, kumbi za mikutano, maji, barabara na madaraja ina mchango katika kuchagiza maendeleo.

Hivyo, kama halmashauri zitatimiza wajibu wake ipasavyo kuhakikisha asilimia 40 za mapato ya ndani zinatengwa, miradi mingi inaweza kuibuliwa na kutekelezwa pasipo kuitegemea zaidi serikali kuu.

Ni muhimu halmashauri kuwa na nidhamu ya hali ya juu katika makusanyo ili zipatikane fedha za kukamilisha miradi ya maendeleo.

Sambamba na hilo, ni lazima pawepo na nidhamu ya kuhakikisha asilimia 40 ya mapato ya ndani haitumiki katika matumizi yasiyo ya miradi ya maendeleo, ili wasikwamishe jukumu hilo.

Kama fedha za miradi ya maendeleo zitatumika katika matumizi mengine, ni dhahiri makusanyo yatakuwapo lakini miradi ya maendeleo haitaweza kutekelezwa kama inavyotakiwa.

Waananchi wana kiu ya kupata maendeleo ili kuboresha ustawi wao. Hivyo ni vyema kiu hii ya wananchi kupata ikakatwa kwa kupelekewa miradi ya maendeleo inayogusa maisha yao. Lakini viongozi wa serikali, wabunge na madiwani wakumbuke walijinadi kwa wananchi wachaguliwe ili wawaletee maendeleo. Ahadi za viongozi hawa zitaweza kutekelezwa kwa ushirikiano wa serikali kuu pamoja na serikali za mitaa kutimiza wajibu wake wa kutenga asilimia 40 ya mapato ya ndani kugharamia miradi ya maendeleo.

Katika kila fedha inayoingia katika mfuko wa halmashauri kama mapato ya ndani, ni vyema wakurugenzi wakazingatia asilimia hiyo ni kwa ajili ya kutekeleza na kukamilisha miradi ya maendeleo katika maeneo yao.

Faida kubwa ya kutenga fedha za mapato ya ndani kugharamia miradi ya maendeleo ni kuongeza mwamko wa wananchi kulipa kodi kwa hiari kwani watakuwa mashahidi wa namna kodi na ushuru wanaolipa ulivyotumika kuwaboreshewa maisha kupitia miradi ya maendeleo.

Kama hakutakuwa na miradi ya maendeleo iliyopatikana kwa mapato ya ndani, ni dhahiri wananchi watakuwa wagumu kulipa kodi na ushuru kwa hiari, jambo litakalokwamisha, kwani kodi na ushuru unaolipwa wananchi ni nyenzo muhimu ya kufikia matamanio yao.

HABARI KITAIFA

# TNBC yawahimiza Diaspora kuwekeza nchini

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Biashara (TNBC) limewahimiza Watanzania waishio nje ya nchi kuchangamkia fursa za kibiashara na uwekezaji zilizomo nchini.

Pia limewashauri na kuwashawishi wawekezaji wengine kuwekeza Tanzania.

Akizungumza kwenye kipindi maalumu cha Redio Kilimanjaro nchini Marekani juu ya uwekezaji wa Diaspora Tanzania, Katibu Mtendaji wa TNBC, Dk. Godwill Wanga, amewataka Watanzania waishio ughaibuni kuelewa kwamba mazingira ya biashara na uwekezaji yameboreshwa sana, na kuwataka waje Tanzania kuwekeza.

"Wakati umefika sasa kwa Watanzania waliopo nje ya nchi kuwa mabalozi wa kutangaza vivutio vya biashara na uwekezaji vilivyomo nchini ili Tanzania ipate wawekezaji wengi na nchi ipige hatua kimaendeleo na kiuchumi," alisema Dk. Wanga.

Alisema kuna fursa za biashara na uwekezaji kwenye sekta za utalii, miundombinu, kilimo na biashara na kuwataka wanadiaspora kuchangamkia fursa hizo na kuwekeza katika sekta hizo ili taifa linufaike na uwekezaji huo.

"Ujenzi wa miradi ya kimkakati ya reli ya kisasa (SGR), Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere ni miradi kwa aina fulani inaohamasisha uwekezaji kwenye hoteli, vituo vya afya na maeneo ya biashara. Uwekezaji katika maeneo hayo kutachochea ukuaji wa uchumi wa nchi," alisema Dk. Wanga.

Ameeleza pia kuwa kuna fursa za uwekezaji kwenye miundombinu ya barabara za mwendokasi, uwekezaji kwenye mifumo ya maji na afya, ujenzi wa maeneo ya biashara katika viwanja vya ndege na kuwataka washirikiane na serikali ili waweze kufanya biashara katika mazingira wezeshi.

Alieleza pia fursa ya uwekezaji kwenye viwanda vya kuunganisha simu na vifaa vyake na aina nyingine za viwanda vya elektroniki na kuongeza kuwa fursa hii inatokana na kuwapo kwa soko kubwa la simu za mkononi Tanzania na nchi nyingine za Afrika. "Tunawaomba Watanzania waishio nje kutangaza vivutio yetu ili kusaidia kukuza ajira kwa vijana na kukuza uchumi wa nchi," alisema.

# Vibali wafanyakazi wa kigeni SGR kupitiwa upya

**Na Frank Kaundula**, MOROGORO

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Vijana na Ajira, Patrobas Katambi, amelitaka Shirika la Reli Tanzania (TRC) kupitia upya vibali vya wafanyakazi katika ujenzi wa Reli ya Mwendokasi (SGR) kutokana na kuwapo kwa wafanyakazi 732 wa kigeni wasio na vibali vya kazi na kusababishia serikali hasara.

Katambi alitoa agizo hilo wakati akikagua maendeleo ya ujenzi huo wilayani Kilosa na kusema wafanyakazi hao wanaisababishia serikali hasara kubwa kwasababu wanatumia hati za kusafiria za kibiashara balada ya kuwa na vibali vya kazi.

Alisema kwa sasa wafanyakazi hao wanalipa kodi ya Dola 200 za Marekani kutokana na kutokuwa na vibali na walitakiwa kulipa Dola 1,000 na kuifanya serikali kupata hasara ya takribani Dola 800 kwa kila mfanyakazi.

"Katika kila mmoja kati ya wafanyakazi 732 tumepata hasara ya dola 800 za kimarekani sasa naagiza kwamba tufanyike utaratibu kukagua upya vibali vya wafanyakazi wote ili tuweze kupata fedha ambazo zitasaidia wananchi katika miradi ya maendeleo," alisema Katambi.

Aliwataka watendaji hao kutoa vibali hivyo kwa utaratibu ulioelekezwa kisheria ili fedha zitakazopatikana zitumike kwenye shughuli za maendeleo nchini.

Awali, akitolea ufafanuzi suala hilo, Kamishna wa Kazi, Brigedia Jenerali Francis Mbindi, alisema kumekuwa na udanganyifu wa wafanyakazi wa kigeni kutumia hati za kusafiria (visa) kama mbadala wa kibali cha kazi jambo ambalo ni kinyume na taratibu za kazi.

Alisema tayari alishaanza kufuatilia baadhi ya wafanyakazi wanaoenda kinyume na sheria za Tanzania katika kupata vibali vya kazi kwa kuwa wengi wanaofanya hivyo wanafanya kwa kujificha.

"Sheria inatambua kwamba mgeni anayekuja kufanya kazi nchini lazima awe na kibali cha kazi kutoka kwa Kamishna wa Kazi, lakini kumekuwa na changamoto ya baadhi ya wafanyakazi au hata waajiri kutumia ujanja ujanja kukwepa wasilipe kodi," alisema.


## Ushauri wa Wadau wa Mitaa kwa shughuli za mradi wa kaboni ya Dhahabu 'RUDI WATER Project'

4Life

**Ndugu Mdau,**

4LIFE Solutions itatekeleza shughuli za mradi wa kaboni VPA2: 'RUDI WATER Project' chini ya Mpango wa Shughuli za Kiwango cha Dhahabu (PoA) Programu endelevu ya Usafi wa Maji. Mradi utasambaza teknolojia salama ya utakaso wa maji, inayoitwa SaWa, kulingana na Teknolojia inayotumia miale ya jua ili Kuzuia Maambukizi ya magonjwaa/maambukizi yanayotokana na unywaji Maji yasiyo masafi kwa kaya zinazoishi katika mikoa ya Shinyanga na Ruvuma (Madama, Namtumbo, Songea, Kahama / Msalala, Shinyanga DC, MbogweWilaya), Tanzania. PoA inasimamiwa na 4Life Solutions (zamani inayojulikana kama SolarSack), iliyo na ofisi kuu Kidenmaki inaanza. Katika muktadha huu Ushauri wa Umma wa Wadau wa Mitaa utafanyika kwa wadau wote wa ndani ya nchi, walioathirika na wanaovutiwa, pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali, vikundi vya wanawake, taasisi za utafiti na mashirika / watu wanaofanya kazi juu ya mada zinazohusiana na shughuli za mradi, watunga sera juu ya kitaifa na ngazi ya wilaya na pia kwa watu wa eneo, jamii na wawakilishi ambao wameathiriwa moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja na mradi huo.

4LIFE Solutions (Waratibu na wasimamizi Taasisi ya PoA) inaalika watu wote wanaopenda kuhudhuria
**Ushauri wa Wadau wa Mtaa mnamo Oktoba 29th, 2021, 8:30 asubuhi hadi 13:00 jioni katika**
**Ruhuwiko Hunt Club**
**Mji wa Ruhuwiko-Songea**
**Mbinga road**
**Tel N ° ya ukumbi+255620655773 AU +255252951008**

Wadau ambao hawawezi kuhudhuria mkutano huo, wana uwezekano wa kushiriki mkondoni kupitia Zoom. Maelezo ya kuingia ni yafuatayo:

Umealikwa kwenye mkutano wa Zoom.
**Wakati: Oktoba 29, 2021 08:30 AM E.A.T (MUDA WA AFRIKA MASHARIKI)**

Jisajili mapema kwa mkutano huu ukitumia kiunga hiki:
**https://us02web.zoom.us/meeting/register/tZAsfuivqT8pG9FuSHs5itwOHbQDg7-5ZN1U**

Baada ya kujiandikisha, utapokea barua pepe ya uthibitisho iliyo na habari juu ya kujiunga na mkutano huo.

### AJENDA

- Mapokezi - Kutia saini orodha ya washiriki (8:30 asubuhi)
- Utangulizi na uwasilishaji wa Mradi (9:00 asubuhi)
- Maswali na maoni juu ya mradi huo (9:30 asubuhi)
- Kanuni za Kulinda Tathmini ya mradi (10:30 asubuhi)
- Tathmini endelevu ya mradi (11:15 am)
- Majadiliano juu ya utaratibu wa malalamiko na ufuatiliaji wa athari za maendeleo endelevu (12:15 pm)
- Fomu za tathmini na kufungwa kwa mkutano (12:30 pm)
- Maonyesho (12:45 pm)
- Chakula cha mchana (13:00 pm)

**www.4lifesolutions.com**

Ikiwa kuna maswali yoyote au ikiwa unataka maelezo zaidi na habari za mradi kabla ya mashauriano, tafadhali andika barua pepe kwaJulius Macharia, Meneja wa Kaboni kutoka 4LIFE Solutions (jkm@4lifesolutions.com) au piga simu kwa Happiness Urasa, Msimamizi wa Miradi nchini Tanzania kutoka 4Life Solutions (+255 767 007 505) Tafadhali tumia maelezo haya ya mawasiliano pia kwa kutoa maoni yako ikiwa huwezi kushiriki katika mkutano wa wadau.

# Waziri atoa siku 14 ukarabati tangi la maji

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

NAIBU Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, ametoa wiki mbili kwa Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Njombe, kuhakikisha tangi la kuhifadhia maji la mradi wa kijiji cha Usililo wilayani Makete linakarabatiwa ili kuondokana na adha ya kumwagika kwa maji.

Naibu Waziri alitoa agizo hilo jana Usililo Kata ya Luwumbu baada ya kukagua tangi hilo na kubaini umwagikaji wa maji huku wananchi wakikabiliwa na kukosefu wa huduma hiyo.

"Meneja nakuagiza ndani ya wiki mbili uhakikishe unarekebisha hili tangi ili maji yasimwagike. Inashangaza mnasema hakuna maji lakini hapa yanamwagika. Naomba mrekebishe ili wananchi wapate maji," alisema Mahundi.

Waziri Mahundi alisema lengo la Rais Samia Suluhu Hassan nikuhakikisha anamaliza kabisa tatizo la maji na kuwa historia.

"Lengo la Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha anamtua ndoo mwanamke kichwani niwaambie wanawake tunzeni ndoa zetu suala la maji linakwenda kuwahistoria na lengo ni kusogeza huduma ya maji karibu na nyumbani," alisema mahundi.


Alisema kuwa tayari serikali imetenga Sh. milioni 85 kwaajili ya kwenda kuongeza vituo vya upatikanaji wa maji safi na salama.

Naye Diwani wa Luwumbu, Felix Kyando, aliishukuru serikali kwa ajili ya kutenga fedha takribani Sh. milioni 150 kwa ajili ya kuondoa tatizo la maji.

Mbunge wa Makete, Festo Sanga, alisema kilio cha wananchikatika jimbo hilo ni upatikanaji wa maji.

"Nimezunguka kata 23 na vijiji 98 kukusanya kero za wananchi lakini kilio chao kikubwa ni maji. Kote huko kero ni maji. Tuna shida na maji kweli kweli," alisema Sanga.

Katika ziara hiyo, Mahundi alizungumza na wananchi wa kijiji cha Utweve na kuwahakikishia kuwa serikali imedhamiria kuhakikisha hakuna kijiji kitakachokuwa na tatizo la maji nchini.




Msimamizi wa Maduka ya Vodacom Kanda ya Ziwa, Maryglory Mtika (kushoto), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 10 kwa Vincent Gratus aliyeibuka mshindi wa promosheni ya Tusua Mapene kwa mwezi wa Agosti, katika hafla iliyofanyika jijini Mwanza jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wapatiwa elimu ubora wa bidhaa

**Na Mwandishi Wetu,** KIGOMA

WAJASIRIAMALI kutoka mikoa mbalimbali nchini waliohudhuria maonyesho ya kitaifa ya viwanda vidogo, wamepatiwa elimu kuhusu taratibu za kuthibitisha ubora wa bidhaa hususani kupitia mpango wa bure kwa wajasiriamali.

Wajasiriamali hao wamenufaika na fursa hiyo kutoka kwa maofisa wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) katika maonyesho hayo yaliyofanyika hivi karibuni wilayani Kasulu, Kigoma.

Katika maonyesho hayo, maofisa hao wa TBS walitoa huduma katika banda la kliniki ya biashara linalosimamiwa na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) lengo likiwa ni kumrahisishia mjasiriamali kupata huduma haraka bila kupoteza muda.

Akizungumza kwenye maonyesho hayo, Kaimu Mkuu wa Kanda ya Magharibi wa TBS, Rodney Alananga, aliwashauri wajasiriamali kuzingatia kanuni za uzalishaji na uhifadhi bora na salama ili kuepuka kupoteza masoko na hasara ya kukutwa na bidhaa hafifu.

Pia aliwashauri kuwasiliana na ofisi ya TBS mara kwa mara pale wanapohitaji msaada wa kitaalamu.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiàno na Masoko wa TBS, Gladness Kaseka, alisema shirika hilo hutoa elimu na mafunzo mbalimbali kupitia midahalo, semina, kampeni, maonesho, runinga, redio na mitandao ya kijamii.

"Huu ni mwanzo kwani Shirika litahakikisha elimu ya viwango inamfikia kila mdau na katika ngazi ya chini kabisa. Leo tupo wilayani kasulu kupitia maonesho, lakini tumeshapita Kakonko,

Kibondo na wilaya zingine zaidi ya 70 Tanzania kupitia kampeni za kuelimisha umma na semina za mafunzo.

Elimu na mafunzo tunayotoa ni bure, Serikali inagharamia kupitia TBS na tuna mpango wa kufika nzima," alisema Kaseka.

Naye Ofisa Masoko wa TBS, Deborah Haule, aliwasisitiza wajasiriamali ambao bado bidhaa zao hazijapatiwa nembo ya bora, kuchangamkia fursa ya bure kwa kutuma maombi ya kutumia alama ya ubora kupitia SIDO ili Serikali iwatambue kama wajasiriamali wadogo na kati.

Alisema wakifanya hivyo wataweza kuhudumiwa bure kwa kuwa bidhaa nyingi wanazozalisha zinaangukia katika kiwango cha lazima, hivyo kulazimika kukidhi matakwa ya viwango kwa mujibu wa sheria.

## CHAURU kujenga ghala la mashine kukaushia mpunga

**Na Julieth Mkireri,** RUVU

CHAMA cha Ushirika wa Wakulima wa Umwagiliaji Ruvu (CHAURU), kimebainisha kuwa na mpango wa kujenga ghala kwa ajili ya mashine ya kukaushia mpunga pamoja na kukobolea litakalokuwa na uwezo wa tani 10,000 kwa gharama ya Sh. milioni 800.

Hayo yamebainishwa jana na Mwenyekiti wa CHAURU, Sadala Chacha, alipokuwa akizungumza na Nipashe ofisini kwake kuhusu utatuzi wa baadhi ya kero za chama hicho.

Alisema ghala lililopo lina uwezo wa kuhifadhi tani 2,500 na halina ubora unaotakiwa na hivyo imekuwa kero ya mara kwa mara inayolalamikiwa na wanachama wa CHAURU.

Sadala alisema katika msimu ujao wa 2021 chama hicho kimejipanga kufanya ukarabati mdogo pamoja na kununua pampu mashine kwa ajili ya kituo cha Msua kuongeza ufanisi na kupungza gharama za uzalishaji.

Mwenyekiti huyo pia alibainisha kuwa katika suala la masoko ya mchele unaotoka CHAURU mipaka imefunguliwa na kwamba viongozi wanaendelea kupambana kupata wanunuzi wakubwa.

"Kwasasa tupo kwenye mazungumzo na mteja kutoka Congo pia tumefanya ushirikiano na Agriterra Tanzania kuhusiana na msaada wa kuunganishwa na masoko pamoja na wafanyabiashara wanaochukua mizigo mikubwa," alisema Sadala.

Meneja wa CHAURU, Victoria Olotu, alisema kwa kutumia michango ya wanachama wamefanikiwa kununua trekta, lakini pia wameongeza huduma ya pembejeo kwa wanachama na sasa wanapata mbolea na mbegu.

Victoria pia alisema kutokana na ubovu wa barabara kutoka barabara kuu ya lami hadi Chauru, wameanza ukarabati kwa kutumia fedha za wanachama kuwezesha usafirishaji wa mpunga kuwa rahisi na wanunuzi kufika bila usumbufu.

## Shinyanga yasuasua chanjo ya UVIKO-19

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKOA wa Shinyanga umetajwa kuwa ni miongoni mwa mikoa 10 ya mwisho hapa nchini kwa utekelezaji wa utoaji chanjo ya UVIKO- 19 kwa wananchi.

Mwakilishi kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Kalidushi Charles, alibainisha hayo juzi mkoani Shinyanga, kwenye kikao cha utekelezaji wa mpango shirikishi na harakishi wa uhamasishaji wananchi kupata chanjo ya UVIKO 19 ndani ya siku 20.

Alisema Mkoa wa Shinyanga bado upo nyuma kwenye utoaji chanjo ya UVIKO 19 kwa wananchi wake na kuufanya kuwa ni miongoni mwa mikoa 10 ya mwisho nchini kwenye utoaji wa chanjo hiyo.

Aidha, aliitaja mikoa mingine ambayo ni ya mwisho kuwa ni Lindi, Singida, Geita, Manyawa, Rukwa, Simiyu, Njombe, Katavi, pamoja na Songwe na kuwataka wakuu wa mikoa hiyo kuongeza kasi ya utoaji chanzo kwa wananchi.

"Naombeni mzipeleke chanjo kwenye maeneo ya machimbo ya madini, masoko, stendi za mabasi, viwandani, vyumba za ibada, vijiwe vya bodaboda, kambi za jeshi, taasisi za umma na binafsi, ili muongeze kasi ya utoaji chanjo ya UVIKO-19," alisema Charles.

Nae Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Philemon Sengati, alisema kutokana na mwitikio mdogo wa wananchi kupata chanjo ya UVIKO -19, mkoani humo ataanza ziara kwenye maeneo ya kimkakati, ili kuhamasisha wananchi kupata chanjo na kuondoa mitanzamo potofu.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Yudas Ndungile, alisema utoaji wa chanjo ya UVIKO -19 katika mkoa huo ulianza Agosti 4, mwaka huu na wananchi waliopata chanjo hiyo ni 6,027, kati ya dozi ya chanjo 25,000 iliyotolewa mkoani humo.

**"Naombeni mzipeleke chanjo kwenye maeneo ya machimbo ya madini, masoko, stendi za mabasi, viwandani, vyumba za ibada, vijiwe vya bodaboda, kambi za jeshi, taasisi za umma na binafsi, ili muongeze kasi ya utoaji chanjo ya UVIKO- 19," alisema Charles.**

# Walia ZSTC kushusha bei ya mafuta ya mchaichai

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WAKULIMA wa kilimo cha mchaichai kisiwani Pemba wamelalamika Shirika la Biashara la Zanzibar ( ZSTC) kuwashushia bei ya mafuta ya mchaichai, licha ya kuwa kuna mahitaji sokoni.

Wakizungumza na waandishi wa habari, walisema, kinachowashangaza ni kwamba soko la mafuta ya mchaichai halijashuka, ingawa wakulima wameshushiwa bei kutoka Sh. 200,000 hadi 120,000, hivyo kuwapa hasara kubwa.

Walisema kuna umuhimu ZSTC kuwaangalia kwa jicho la huruma kwa kuwa wamekuwa wakifanya kazi kubwa, huku wakiajiri vijana wa kuwasaidia, na kwamba kwa sasa wameshindwa kurudisha hasara na kushindwa kuwalipa wasaidizi.

"Kwa kweli tumeingiwa na ugonjwa wa shinikizo la damu (presha) kwa sababu tumeajiri vijana ili tuwalipe baada ya mavuno, lakini matokeo yake kwa bei tuliyopangiwa kuwauzia ZSTC hatupati kulipa gharama tulizotumia wala hazikidhi kuwalipa vijana hao, ni mtihani kwetu," alieleza mmoja wa wakulima.

Walieleza kuwa soko la kimataifa lita moja ya mafuta ya mchaichai wananunua kwa shilingi 320,000, ingawa shirika linanunua kwao kwa shilingi 120,000 jambo ambalo linawatia unyonge, kwani wao ndio wanaofanya kazi kubwa.

Walisema mwanzo shirika lilikuwa linanunua kwao lita moja kwa shilingi 200,000 na wao wanapata faida ya shilingi 120,000, lakini kinachotushangaza limewashushia wakati soko halijashuka bei, hivyo wamepata hasara kubwa na twanadaiwa.

Khamis Ramadhan Faraji, mwenye shamba l Mbiji mkoani, alisema walihamasishwa kulima mchaichai, ingawa kwa sasa wameanza kuwavunja moyo kutokana na bei waliyowekewa.

"Sisi ndio tunaofanya kazi kubwa, tunawalipa watu watusaidie, lakini kinachotushangaza na kutusikitisha ni kuona shirika wanachukua wao kwa fedha nyingi kuliko sisi wakulima, hii sio haki kutokana na kuwa soko la bidhaa hiyo halijashuka," alisema.

Alisema, shamba lake lina ukumbwa wa ekari 3.5, ambalo huzalisha mafuta mengi baada ya mavuno, ila kinachowasikitisha ni wameanza kuondolewa matumaini waliyokuwa nayo kutokana na zao hilo.

Salma Said Rashid, mwenye shamba la mchaichai Chonga Wilaya ya Chakechake, alisema, wamekuwa wakipata hasara kutokana na kushuka kwa bei na kukosekana kwa kiwanda cha kukamulia mafuta hayo.

Asha Juma Rihan, mwenye shamba lenye ukubwa wa ekari saba Pujini Pemba, alisema, hadi kukamilisha upandaji wa bidhaa hiyo ametumia takribani shilingi 2,000,000.

"Gharama ya ushughulikiaji bidhaa hii ni kubwa sana, mara zote natumia zaidi ya milioni mbili, lakini nilikuwa napata faida, ila kwa sasa hata gharama hatuwezi kuzilipa.

Mkurungezi Mwendeshaji wa ZSTC, Said Seif, alisema shirika lina ulazima wa kununua mafuta ya karafuu na vitu vitokanavyo na karafuu na sio ya mimea mengine, hivyo ikiwa kuna sehemu wanahisi watapata pesa za ziada wakauze bidhaa yao.

"Sisi tunanunua pale tunapokuwa na uhitaji na huwa tunauza ujazo mdogo mdogo katika soko la ndani na sio la kidunia, kwa hiyo mkulima ana hiari kwenda kuuza ambapo atapata bei kubwa, hawajakatazwa," alisema.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kimataifa ya Misheni Union, Mch. Hildon Mbogela (kushoto), akipokea risala ya wahitimu wa darasa la saba wa Shule ya Misheni ya Bethel ya Mabibo Makuburi, mkoani Dar es Salaam juzi, iliyowasilishwa na dada mkuu wa shule, Theresia Mpemba, wakati wa mahafali ya 17 ya shule hiyo. Katikati ni Mwalimu Mkuu Msaidizi, Charles Mangwe. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Asasi zatakiwa kutatua vikwazo kwa wananchi

**Na Beatrice Shayo**

RAIS wa Taasisi ya Foundation for Civil Society (FCS), Dk. Stigmata Tenga, ameziagiza asasi za kiraia kushikamana kuhakikisha zinatatua vikwazo kwa wananchi.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa mpango mkakati mpya wa mwaka 2022/26, ambao umelenga kusaidia asasi za kiraia kutoa huduma katika jamii.

"Malengo yetu ni kuleta mabadiliko kwa wananchi wa kitanzania na kuwafanya wawe madereva wa maendeleo yao, azma hiyo imetimia. Tukasema hatutachoka tunatamani tuendelee na kushirikiana na wengine kutimiza ndoto yetu ya muda mrefu," alisema Dk. Tenga.

Dk. Tenga alisema wanaanza kwa kuhakikisha wanajenga uwezo na kupima matokeo kwa asasi za kiraia.

Alisema hivyo wakaamua kijikita katika eneo la kuhakikisha wanawajenga wananchi kupitia asasi za kiraia ikiwa ni sehemu ya kuwasaidia kupata maendeleo.

"Afrika tuna mifumo ya kujenga umoja ambayo ilikuwa inajengwa kwenye mifumo ya binadamu eneo la ushirikiano tulilolona lina mapungufu yake, lakini hatuwezi kuliacha tuendelee nao hii sekta ni pana na ina ukubwa inabidi ijengwe na mikono mingi na kwa umahiri mkubwa," alisema Dk. Tenga.

Dk. Tenga alisema matatizo ambayo asasi za kiraia inakumbana nayo yamejikita katika mifumo na wamekuwa wakiyatatua kwa kutumia mbinu za zamani ambazo siyo za kujenga mifumo.

Mkurugenzi Mtendaji wa FCS, Francis Kiwanga, alisema wamezindua mpango mkakati mpya wa FCS ambao unalenga kushuka chini hususani vijijini katika kuwasaidia wananchi.

Alisema kupitia mpango huo taasisi yao itaendelea kufanya kazi na asasi mbalimbali za kiraia ambao ndiyo wadau wao muhimu katika kuwafikia wananchi.

Alisema falsafa ya taasisi yao inaamini kuwa umaskini, hali ya kutokuwa na haki katika jamii, hali ya ukandamizaji watu wengine ni tatizo kubwa na ni adui mkubwa wa maendeleo.

Alisema katika rasilimali zao takribani asilimia 90 inakwenda vijijini kuhudumia wananchi.

Kiwanga alisema katika mpango wao wanazingatia usawa wa kijinsia, kufanya kazi na wadau wao kwa kuwapa heshima inayostahili na kuwaheshimu.

# Tanga yatajwa kuwa Jiji la kimataifa kwa usafi

**Na Joseph Mwendapole,** TANGA

MRADI wa kukusanya taarifa na takwimu za Mkoa wa Tanga uliopewa jina la Livinglab Innitiative, unatarajiwa kulifanya jiji hilo kuwa la kimataifa kwa usafi wa mazingira na taarifa zake kuanza kupatikana kidijitali.

Mradi huo wa miaka mitatu unatekelezwa kwa pamoja na Jiji la Tanga, Chuo Kikuu Ardhi (ARU) na Tanzania Data Lab kwa ufadhili wa Foundation Botnar ya Uswisi.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa Tanzania Data Lab, Stephen Chacha, wakati akizungumza kwenye kikao na madiwani wa Tanga na wadau mbalimbali kuhusu kuboresha taarifa na takwimu zilizokusanywa kwenye kata tisa za mkoa huo ambazo mradi huo unatekelezwa.

Kata hizo tayari zimepokea ramani za kidigitali zinazoonyesha taarifa za maeneo na mifumo taarifa za kijografia (GIS) ili kusaidia kuboresha huduma za ukusanyaji taka ngumu na utambuzi wa maeneo hatarishi.

Chacha alisema ramani hizo ambazo zimetengenezwa na wanafunzi wa ARU pia zinaonyesha taarifa za maeneo muhimu, mitaa na majengo pamoja na mifumo ya kusimamia mipango ya maendeleo ya Jiji la Tanga.

Alitaja kata hizo kuwa ni Chumbageni, Central, Ngamiani Kaskazini, Ngamiani Kusini na Ngamiani Kati, Majengo, Usagara, Duga na Nguvumali.

Chacha alisema mradi huo wa Livinglab Initiative una lengo la kuwezesha matumizi ya taarifa hizo na takwimu kufanya maamuzi mkoani Tanga.

Chacha alisema mbali na kulipaisha Jiji hilo kimataifa pia unatarajiwa kuibua fursa mbalimbali za kiuchumi kwa vijana wa mkoa huo ambao wamekuwa wakishirikishwa kila hatua ya mradi huo.

Alisema vijana waliotumika kukusanya taarifa na takwimu hizo ni kutoka Chuo Kikuu Ardhi ARU na vijana wa Mkoa wa Tanga.

Alisema vijana hao wamefanyakazi kubwa na kwa ufanisi wa hali ya juu kuibua fursa mbalimbali za Mkoa wa Tanga na kutoa takwimu na taarifa ambazo zitakuwa msaada mkubwa kwenye mipango miji.

Alisema kabla ya kuanza kwa mradi huo Jiji la Tanga lilikuwa katika hali mbaya kimpangilio lakini baada ya mradi huo mtu anaweza kutafuta mtaa na taarifa mbalimbali za Mkoa huo kiganjani mwake.

"Sasa hivi unaweza ukaingia kwenye simu yako ukatafuta taarifa mbalimbali za Mkoa wa Tanga, mitaa imeanishwa na kila nyumba na inatumika kwa biashara gani viko mtandaoni," alisema.

Naibu Meya wa Jiji la Tanga, Joseph Colyvas, alisema mradi huo ni muhimu kwani umeliweka Jiji la Tanga kwenye ramani ya dunia.

Alisema mradi huo umeibua mambo mengi zikiwano sehemu ambazo sisalama, maeneo ya wazi, maeneo ya utupaji taka hali ambayo itasaidia hata kupunguza migogoro ya ardhi.

" Botnar wametuambia leo kwamba kuna bilioni 7 zinatarajiwa kuletwa kwa ajili ya maendeleo ya Tanga tunawashukuru sana kwani hadhi ya Jiji letu itapaa na pengine kuyapita majiji mengine," alisema Naibu Meya.



Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Prof. Zacharia Mganilwa (kushoto), na Mkurugenzi wa Kampuni ya TRES Consult (T) Limited, Bashiru Abdul, wakibadilishana mikataba waliyotia saini jijini Dar es Salaam, wa kufanya Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii (ESIA) ili kuruhusu ujenzi wa majengo manne ambayo yatakuwa mahususi kwa mafunzo ya anga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kahama waanza ujenzi madarasa

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MBUNGE wa Kahama (CCM), Jumanne Kishimba, ameanza kuhamasisha wananchi katika kata zao juu ya kushiriki katika ujenzi wa vyumba vya madarasa ili kupokea wanafunzi watakaojiunga na kidato cha kwanza mwakani.

Katika Jimbo la Kahama serikali imeanza kujenga vyumba vya madarasa katika shule sita kwa kushirikiana na nguvu za wananchi pamoja na usaidizi kutoka katika ofisi ya mbunge ili kuhakikisha mwakani hakuna mwanafunzi atakayekosa nafasi ya masomo kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa.

Kishimba aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na wananchi wa Kata ya Malunga katika Manispaa ya Kahama ili waanze ujenzi wa shule mpya ya sekondari ya kata hiyo.

Alisema kuwa kuna shule ambazo zinahitaji usaidizi ili ziweze kukamilisha ujenzi wa madarasa na kwamba yeye amechangia Sh. milioni 1.2 kwa ajili ya ujenzi wa shule ya sekondari na msingi katika kata hiyo.

Aidha, mbunge huyo alitoa Sh. 700,000 kwa ajili ya kulipa fundi katika shule ya sekondari ya Igomelo, Sh. 400,000 kwa Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kahama mjini ambao nao wameamua kushiriki katika kuongeza madarasa katika shule ya sekondari ya Malunga.

Baadhi ya wananchi wa kata ya Malunga walisema kuwa wakati umefika sasa kwa serikali kuleta sera ya ujenzi wa madarasa yanayochukuwa wanafunzi 50 kwani kwa sasa ukubwa wa madarasa ni mdogo haulingani na idadi ya wanafunzi hali ambayo inafanya wananchi kujenga madarasa mengi.

Mmoja wa wananchi hao, Komanya Nkwabi, alisema kuwa madarasa yakijengwa makubwa kutakuwa na unafuu wa utendaji wa kazi kwa walimu huku akiongeza kuwa kama shule hiyo itakamilika kwa wakati itanufaisha wananchi wa maeneo husika katika kata hiyo.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Malunga, Emmanuely Mrossa, alisema katika ujenzi wa sekondari hiyo jumla ya Sh. milioni 66.1 zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa maboma huku wananchi wakitoa vifaa, mawe, mchanga, moramu, kokoto na saruji vyenye thamani ya Sh. milioni 3.1.

# SBL kuwekeza zaidi kwenye uchumi, jamii

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) imesema itafanya uwekezaji zaidi wenye tija kwa biashara zake za nchini ili kuendelea kuchangia maendeleo ya nchi kupitia kulipa kodi na kuzalisha ajira.

SBL inamiliki viwanda vitatu vya kuzalisha bia vilivyopo katika mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro na Mwanza pamoja na kiwanda kimoja cha kuzalisha pombe kali kilichopo Moshi pia mkoani Kilimanjaro.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wakati wa kiwanda kipya cha kuzalisha pombe kali kilichopo Moshi, Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti, alisema katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita kampuni ya SBL imewekeza kiasi cha shilingi bilioni 166

Ocitti alisema kiasi hicho cha fedha kimehusisha upanuzi wa viwanda vyake vya Dar es Salaam, Moshi, Mwanza pamoja na ujenzi wa kiwanda cha kisasa cha kuzalisha pombe kali ambacho kimeifanya kampuni hiyo kuwa kati ya wazalishaji wakubwa wa pombe kali wa ndani.

"Uwekezaji pamoja na upanuzi wa biashara zetu umekuwa na faida kubwa kwa Tanzania kwa kuwa umepelekea kuongezeka kwa mahitaji ya malighafi ambazo tunazinunua kutoka kwa wakulima wa ndani.," alisema mkurugenzi huyo.

Alifafanua kuwa uwekezaji wa SBL pia umetengeneza ajira mpya na pia umeiwezesha kampuni hiyo kulipa kodi zaidi kwa serikali na kuongeza kuwa kampuni hiyo itaendelea kuwekeza na kutengeneza fursa za zaidi kwa Watanzania.

Kwa upande wake Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, aliipongeza SBL kwa uwekezaji mkubwa ambao imekuwa ikiendelea kuufanya hapa nchini na kusema serikali itaendelea kutengeneza mazingira mazuri ya kuwekeza na kufanya biashara kwa sekta binafsi.

"Kwa namna ya pekee napenda kuipongeza kampuni ya SBL kwa kufanya kazi na wakulima wa ndani kupitia programu yake ya kununua nafaka ambapo inanunua asilimia 80 ya nafaka zinazohitajika kwa uzalishaji wa bidhaa zake kwa wakulima wa ndani katika mikoa ya Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Mwanza, Morogoro, Mara, Singida na Dodoma. Natoa wito kwa makampuni mengine kuiga mfano huu," alisema.

Kupitia biashara zake nchini, SBL imetoa ajira za moja kwa moja kwa zaidi ya watu 800, huku ikitoa maelfu ya ajira zisizo za moja kwa moja kwa maelfu ya watu kupitia mnyororo wake wa thamani.

Rais Samia na kinamama marais wa Afrika, waanze na kumaliza shida hizi



Ukurasa 12

siasa

JUMATANO SEPTEMBA 29, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe



Ukurasa 14

**KANSELA MSTAAFU ANGEL MARKEL;**
**Mama wa kwanza kwenye wadhifa wenye nusu ya historia yake kisiasa**

# KIKAO MSAJILI, POLISI, VYAMA...

- Mkanganykio waibuka kila pande na dhana yake
- Wanaodai kususa watahadharishwa 'itakula kwao'

**Na Sabato Kasika**

MWEZI ujao, Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, anatarajia kukutana na viongozi wa vyama vya siasa na Jeshi la Polisi, ili kuondoa mvutano kati ya ofisi yake, vyama na polisi

Hata hivyo, wakati akiwa ametangaza nia hiyo, viongozi wa baadhi ya vyama wameshatangaza kususia kikao hicho, hali inayoonekana kuwa huenda ikaathiri kufikiwa lengo.

Wanaotangaza kususia kikao ni CHADEMA, NCCR-Mageuzi, CUF na ACT-Wazalendo, ambao wanatoa sababu za kutoshiriki.

**KWANINI KUSUSA?**

Mkurugenzi wa Itikadi, Uenezi na Mambo ya Nje, John Mrema, anasema, CHADEMA haiko tayari kukutanishwa na Jeshi la Polisi, kama ambavyo ametangaza msajili huyo.

Mrema anaituhumu polisi, akidai kwa mambo ambayo wamekuwa wakiyafanya kwa miaka sita, ni uhalifu ambao unastahili kufikishwa mahakamani.

Mkuu wa Idara ya Uenezi na Uhusiano ya Umma wa NCCR-Mageuzi, Edward Simbeye, anasema, kikao hicho hakina umuhimu wowote kwao.

Katika ufafanuzi wake anadai msajili ni mtendaji na polisi ni utekelezaji na lakini hakuna mtunga sera, hivyo hawaoni sababu ya kwenda kukaa kujali mambo yanaruhusiwa kikatiba.

Mwenyekiti wa CUF Taifa, Profesa Ibrahimu Lipumba, anasema kutokana na mwingiliano wa tarehe chama hakitakuwa na nafasi, kitakuwa kwenye kongamano la Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD).



Katibu wa Habari, Uenezi, Uhusiano na Umma wa ACT-Wazalendo, Salim Bimani, **PICHA: MTANDAO**

Anafafanua kuwa hawana taarifa rasmi kutoka kwa msajili mbali na kusikia kwenye vyombo vya habari.

Wakati vyama hivyo vikitoa sababu hizo, ACT-Wazalendo, inasema, baada ya kutafakari kwa kina, imeamua kuwa haitashiriki kikao hicho kwa kuwa ratiba imeingiliana na vikao vya viongozi wakuu wa chama hicho.

Katibu wa Habari, Uenezi, Uhusiano na Umma wa chama hicho, Salim Bimani, anasema, Oktoba 21 na 22, viongozi wakuu wa chama hicho watakuwa kwenye mkutano mkuu wa kitaifa wa haki, amani na unaoandaliwa na TCD.

Aidha, anataja kutopatiwa mrejesho wa barua waliyoituma kwa msajili huyo kuomba kikao hicho kimshirikishe Waziri wa Mambo ya Ndani na pia matamshi ya baadhi ya viongozi wanaotarajiwa kukutana nao.

Bimani anasema, kauli ya IGP kuwa hakuna shida ya mikutano ya nje, bali tatizo lipo kwenye mikutano ya ndani na inabidi sheria iwekwe sawa, ni dalili kuwa huenda mkutano, ukatumika kubinya zaidi shughuli za kisiasa.

Baada ya maelezo ya vyama, Nipashe inazungumza na baadhi ya wadau wa siasa na wachambuzi kupata mitazamo yao.

**KIKAO HAKINA NGUVU**

Mchambuzi Gwandumi Mwakatobe anasema, sheria na katiba ya nchi vinaruhusu mikutano ya vyama vya siasa, hivyo haoni umuhimu wa kuitisha kikao, kwa madai kwamba hakina nguvu kuliko katiba.

Gwandumi anasema, ingekuwa vyema kama msajili angetumia nafasi hiyo kuwalekeza polisi kufuata sheria na katiba, ili vyama vya siasa viendelee na shughuli zake kama kawaida, kwa kuwa vipo kisheria na kikatiba.

"Hicho ndicho ninachashauri, kwani kipo kisheria na kikatiba, kikao chake hakiizidi katiba wala sheria," anasema Mwakatobe.

Anataja njia nyingine ya kuweka mambo sawa kwamba ni msajili kuwa na utaratibu wa kufanya mikutano ya mara kwa mara kati yake na vyama vya siasa kwa lengo la kusimamia ili kila upande utimize wajibu bila kugombana.

Anasema njia hiyo itawafanya polisi kuendelea na kazi ya kuzuia vurugu kwenye mikutano ya siasa, ambayo ipo kisheria badala ya kuisambaratisha, kukamata na kuwaweka watu ndani.

**SI VIZURI KUSUSIA**

Mwanasiasa na kada wa CCM Thomas Ngawaiya anasema, Msajili wa Vyama vya Siasa ni mlezi wa vyama hivyo, na kwamba si vyema vyama kumsusia.

"Sheria ya namba tano ya vyama ya mwaka 1992 inaruhusu kuwapo kwa mikutano ya hadhara, lakini haifuatwi, kwa hiyo ingekuwa vyema kama vyama vyote vitahudhuria kikao hicho ili kuwekana sawa," anashauri.

Ngawaiya anasema, katika kikao hicho, viongozi wa vyama vya siasa watakuwa na nafasi ya kuhoji kinachokwamisha sheria isifuatwe ili wapate majibu ya utata huo ambao umesababisha msuguano kati yao na Jeshi la Polisi.

"Wasipohudhuria itakuwa imekula kwao, kwa sababu watakuwa wamepoteza nafasi ambayo wangeitumia kuhoji na kuelezea dukuduku lao kwa Jeshi la Polisi ambalo wamekuwa wakigombana nalo kila mara," anasema.

Kada huyo wa CCM anaongeza kuwa, kikao hicho si cha vyama vya upinzani tu bali hata chama kwa kuwa nacho kinalelewa na msajili na kwamba vyama vyote visipange kukosa nafasi hiyo.

**INAENDELEA UK.12**



Makamu wa Rais wa Sudan, Rebecca Nyandeng De Mabior, alihutubia mkutano UN. **PICHA: MTANDAO.**

# Rais Samia na kinamama marais wa Afrika, waanze na kumaliza shida hizi...

**Na Gaudensia Mngumi**

WANAWAKE viongozi wa Afrika mwezi huu, wametikisa Baraza la Umoja wa Mataifa, wakihutubia na kuzungumzia suala la kuondoa watu kwenye umaskini na ugonjwa wa COVID-19.

Rais Samia Suluhu Hassan, katika hotuba yake aliyoitoa UN, anasema tatizo la COVID-19 limeonyesha tofauti kubwa kati ya mataifa na kwamba nchi zilizoendelea zinatoa chanjo ya pili, lakini nchi maskini kama Tanzania hazijaweza kuchanja hata asilimia mbili ya raia wake.

Anasema hatua za uchanjaji zilivyo leo, inaelekea itakuwa vigumu kutimiza kiwango cha Shirika la Afya Duniani (WHO) cha kila taifa kuchanja angalau asilimia 40 ya raia wake kufikia mwisho mwa 2021 na angalau asilimia 70 katika miezi sita ya mwanzo ya 2022.

Rais Samia anazungumzia suala la kuwa na usawa wa kijinsia na kuhimiza kuwapo na misaada na ushirikiano wa kusaidia kuwaondoa kwenye lindi la umaskini wanawake na mabinti wa Tanzania.

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Gambia, Isatou Touray, kama alivyofanya Rais Samia amehutubia UN na kukumbusha kuwa dunia ni moja na UN ni eneo ambalo wote wanakutana kujadiliana na kupata ufumbuzi wa matatizo yaliyopo na kutaka hali hiyo iinufaishe Afrika

Mariam Chabi Talata, kutoka Jamhuri ya Benin, anatoa hutuba kwenye mkutano wa UN, akizungumzia kuwa na Afrika inayobadilika.

Makamu wa Rais wa Sudan Kusini, Rebecca Nyandeng De Mabior, analisemea taifa changa kuliko yote duniani, kwenye mkutano huo.

Anaonyesha namna kinamama viongozi wa Afrika walivyo na uchungu, akisema inauma kuona nchi yenye rasilimali nyingi na utajiri wa ardhi kama Sudan inaitwa maskini.

Anasema Sudan ina changamoto ya vijana na wanawake wake kupata mbadala wa maisha badala ya kuendelea kushika bunduki na silaha na kuendeleza janga la kuangamizana.

Licha ya kwamba hakuwapo kwenya Mkutano wa 76 wa Baraza la Usalama, Rais Sahle-Work Zewde, wa Ethiopia, aliyeanza kazi hiyo Oktoba 2018, ni kinamama viongozi wa bara hili wanaoyafahamu madhila ya umaskini na unyanyasaji kijinsia.

Kuwapo viongozi wanawake Afrika ni mwamko unaohamasisha Waafrika kuungana, kuleta mawazo mapya na ukombozi unaoheshimu mchango wa kila raia.

Sauti za wanawake kwenye uongozi na kuhimiza kuwapo usawa wa kijinsia kama anavyosema Rais Samia ni muhimu kutatua changamoto nyingi.

Kwanza ni bara lenye vilio vya kuporwa maliasili zake, kuvamiwa na mitandao ya wahalifu, wauzaji na kuwalisha vijana wake dawa za kulevya.

Aidha, ni kituo cha wakwepa kodi tena wanaosaidiwa na viongozi na taasisi za umma. Kusini ya Jangwa Sahara, Afrika imejaa bidhaa feki na bandia na hadi leo inaendelea kuuza malighafi kwa miongo mingi hata baada ya uhuru.

Changamoto kwa kinamama viongozi hawani kwamba licha ya kuwa na rasilimali nyingi imekuwa ni dunia ya watu wenye madeni makubwa wanaodaiwa na Ulaya, China na Marekani, yote haya wanatakiwa kusaidia kupata ufumbuzi.

Viongozi wanawake waanza kubadilisha hali duni iliyoko na kuifanya Afrika imara na bora kwenye afya, waukumbushe Umoja wa Afrika (AU) kuwa mwaka 2001 miongo miwili iliyopita walikubaliana katika kikao cha wakuu wa nchi kutenga asilimia 15 ya bajeti ya nchi zao kwenye sekta ya afya.

Kama Rais Samia, alivyosema kitisho cha COVID-19, ni kikubwa, lakini kama azimio hilo lingetekelezwa huenda changamoto za afya duni zingepungua na nchi zingeweza kununua chanjo ya UVIKO-19.

Ni jukumu la wanawake hao viongozi kuwaondoa mabinti kwenye udhalilishwaji, utumwa wa ujinga na kukosa elimu, kuolewa na kupata mimba utotoni.

Afrika itafurahishwa na viongozi kinamama kwakuona si wanawake viongozi peke yao bali pia wanawaibua wanawake wajasiriamali, wanazuoni, wanaharakati na watu wenye uwezo kuleta maendeleo na walio chachu ya madiliko ya kweli.

Kinamama viongozi waonyeshe njia ya kuwakomboa vijana ili wawe wabunifu na wagunduzi, viongozi, wachapakazi na watu wanaoamini kuwa vijana ni msingi na mhimili wa maendeleo ya Afrika.

Tatizo la umeme na maji Afrika ni kubwa kinamama viongozi wajitume kulipunguza. Kama kuna baraka ya jua mwaka mzima na upepo usiokoma kuna haja ya Afrika kubakia gizani?

Wanawake viongozi waonyeshe njia ya kupata haki na usawa kwakila raia, ajira mpya, kuzalisha na kujitosheleza kwa chakula na aina mpya ya maendeleo ya uchumi itakayoacha alama ya kudumu.

Waonekana kwenye AU wakitaka kuwapo na uwajibikaji, mabadiliko na kushinikiza kuboresha maisha ya Waafrika kwaushirikiano na asasi za kiraia, wasomi na, wanadayaspora na wananchi kuondoa ukanadamizwaji wa kiuchumi, kisiasa na kitabibu unaoonekana leo kuwa mataifa yaliyoendelea yamechanja raia wake chanjo ya COVID-19 zaidi ya mara moja wakati Waafrika zaidi ya bilioni 1.2 hata theluthi moja haijachanjwa.

# KIKAO MSAJILI, POLISI, VYAMA...

**INAENDELEA UK.11**

**VYAMA VIKO SAHIHI**

Kwa upande wake mchambuzi mwingine wa siasa Dk. Dinnah Mbaga, anasema vyama ambavyo vimesema havitahudhuria kikao hicho, viko sahihi kwa kuwa polisi hawahusiki katika kikao hicho.

"Njia ambayo ingefaa, ni msajili kukutanisha vyama na Waziri ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwani polisi si waamuzi, bali watekeleza maagizo, hivyo kuwashirikisha katika kikao ninaona si sahihi," anasema Dk. Mbaga.

Anafafanua kuwa kuwashirikisha polisi kwenye kikao hicho ni sawa na kuwachanganya wanasiasa, na kwamba ndiyo maana baadhi yao wametoa sababu za kukikataa.

"Ushauri wangu unaelekezwa kwa msajili wa vyama kwamba, yeye aachane na polisi, badala yake aelekeze kwenye wizara yenyewe ambayo ndiyo inayotoa maagizo yanayotekelezwa na polisi," anasema.

Anasema, utaratibu huo ukitumika, vyama vinaweza kuhudhuria na kutoka na maazimio yatakayokuwa na manufaa kwa pande zote, kuliko ilivyo sasa ambapo baadhi vimeanza kuonyesha kutokuwa na imani na kikao hicho.

**NI FURSA NZURI**

Said Msonga ni mchambuzi, anayesema tofauti zinapojitokeza zikiwamo za kisiasa, kwa kawaida meza ya mazungumzo ni fursa nzuri ya kuzimaliza na kufungua ukurasa mpya, hivyo vyama visisuse.

"Kikao kilichoitishwa na Jaji Mutungi ni fursa kumaliza sintofahamu ambayo imekuwapo kwa muda mrefu kati ya polisi ya wanasiasa, hivyo ingependeza kama viongozi wa vyama watahudhuria," anasema Msonga.

Anafafanua, inawezekana polisi wakawa wako sahihi wanapozuia mikutano ya vyama vya siasa, au wakawa wanakosea, na kwamba kikao hicho kitajadili na kila upande utoe maoni yake.

"Wasipofanya hivyo, maana yake suala hilo haliwezi kupatiwa ufumbuzi na badala yake malumbano yataendelea, lakini ninamini kwamba meza ya mazungumzo inaleta matokeo mazuri," anasema.

Katika ufafanuzi wake anasema, huenda suala likawa ni dogo hasa kwenye tafsiri na mtazamo, ambavyo vyote vinaweza kuwekwa sawa iwapo vyama vitaitikia wito wa msajili bila kujali yaliyotokea nyuma.

# Chongolo anapoitikisa Kusini

## • Akerwa uhusiano mbovu ndani ya CCM
## • Ashangaa kuwachukia wabunge, madiwani

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa NJOMBE**



TIMU ya Sekretarieti ya CCM ikiongozwa na Katibu Mkuu, Daniel Chongolo, baada ya kuzuru mikoa ya kusini, imeitaja changamoto kubwa inayokitafuna chama chao kuwa ni uhusiano mbovu ndani ya CCM.

Wajumbe wa Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM akiwamo Chongola na Katibu wa Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, wametembelea mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma na Njombe , wakilenga kukutana na wananchi na wanachama ili kuwakumbusha viongozi wajibu wao wa kutatua kero za Watanzania.

Akizungumza katika ziara hiyo, Katibu Mkuu Chongolo (pichani), anasema changamoto iliyomkera ni mahusiano mabovu ndani ya chama hicho kila walipopita.

"Kila tulipopita kwa viongozi wa serikali mahusiano yao yapo vizuri tatizo lipo ndani ya chama jambo ambalo haliwezi kuvumiliwa." Anaahidi.

"Hawa jamaa wa serikali wanakwamishwa na sisi chama, japo wana matarajio ya kuhakikisha mambo yanakwenda kwa kasi tunawaangusha. Kinachosikitisha na kuaibisha wapo wengine ni watendaji tuliowapa majukumu ndani ya chama wanashiriki kuwavuta nyuma wenzao. Hii sio sawa," anaongeza.

Chongolo anataka mabadiliko ya haraka na viongozi waache mchezo wa majungu wawasaidie na kushirikiana na viongozi wa serikali kutekeleza ilani ya uchaguzi wasiwakwamishe na wala wasiwakwaze.

**CHUKI Vs MBUNGE, DIWANI**

Anakemea kuendeleza fikra za mgombea wangu licha ya kwamba uchaguzi umemalizika, akisema mwaka jana ulifanyika uchaguzi na sasa umekwisha.

"Uchaguzi ulifanyika hapa kama hukumtaka mtu ilikuwa ni wakati muafaka wa kusema huyu simhitaji lakini kama alipitishwa na wananchi vikao vikamwidhinisha akachukua fomu huyo ni mgombea wa kila mmoja kama alikuwa mbunge au diwani ndiye kiongozi wetu. Wakati wa kutengeneza wabunge ama madiwani bado imebakia miaka minne. Tunasubiri uchaguzi wa ndani wa chama chetu," anawaambia.

"Ni lazima tubadilike sasa kwenye chama shida ni ipi? Uchaguzi umekwisha mwaka jana bado kuna mtu ana ndoto ya nafasi? Tuna uchaguzi mwingine wa ndani mwakani mnagombana na watu waliokwenda kwenye dola kufuata nini? Mnagombea nini?"Anahoji Chongolo.

Anaongeza: "Hawa wabunge si mmewapigia kura, kama humpendi mbunge subiri 2025 sasa hivi chokochoko kwenye majimbo ya nini? Chokochoko za nafasi za nini? Wameshachaguliwa tuwaache wafanye kazi tutawapima kwa kazi waliyoifanya mwaka 2025 . Tukihangaika kuwachokonoa sasa hivi au kuwafuatilia na kuwazushia tutafika mwaka 2025 tukiwa na majeraha badala ya kutafuta ushindi."

"Wanaowasumbua sisi tunawaona na wanaopiga kelele tunawajua chama hiki kina macho marefu tunaona kila kitu. Kila mtu ana haki katika chama lakini hana haki ya kusumbua na kuvuruga aliyeshinda uchaguzi," anawaonya.

Anataja wilaya moja walikofika na kukuta figisu kwa mbunge ambaye kila akifika anazuiliwa kutekeleza kazi za jimbo matokeo yake maendeleo hayaendi jambo analowaambia halikubaliki.

Chongolo anaongeza :"Tatizo lipo kwako unayekubali kununuliwa na kuwa mfuasi wa mtu fulani jambo ambalo linaweza kusababisha kupatikana na viongozi ambao hawana sifa ifike wakati tuanza kuwaogopa watu wanaoandaliwa kuwa viongozi."

Anasema ni aibu chama kinachounda serikali kubaki na misuguano isiyo ya maana na kuonya kuwa wananchi wanawadharau.

**MASLAHI BINAFSI**

Katibu Mkuu wa CCM anasema maeneo mengi katika wilaya walizozitembelea hali si shwari kwa sababu ya maslahi binafsi, katibu anapelekwa akifika katika eneo badala ya kufanya kazi ya utumishi anafuata matakwa yake , na kuonya kuwa wanaofanya hivyo wanataka wawe miungu watu na kila mmoja awasikilize wao?

"Wewe umechaguliwa kuwa mwenyekiti, mwenezi, ama nafasi nyingine za kamati ya siasa kazi yako kila wakati ni kutoa maneno huku na kupeleka kule. Unatupa mashaka wewe unayepata kazi ya ziada ya kutoa maneno ukiona kiongozi yupo 'bize' kutengeneza majungu kwa wengine fahamu hafai kuongoza," anaonya Chongolo.

Anasema wanaojiona wana maneno wajitathimini na waondoke kwenye chama waje watu wengine wenye dhamira ya kazi.

**JICHO MAALUMU LINDI**

Chongolo anasema katika maeneo ya Lindi kuna changamoto ya gari la wagonjwa katika vituo vya afya na kuahidi kulifanyia kazi ili wananchi wapate huduma kwa wakati.

"Kiukweli nimeshuhudua mwenyewe Lindi inahitaji kuangaliwa kwa jicho maalum hasa kwenye maeneo matatu kwanza miundombinu ya barabara, maji, mawasiliano na kwenye suala la umeme tayari fedha zimeshatolewa wakandarasi wanatakiwa kutekeleza majukumu yao kwa wakati," anasema.

Anaongeza kuwa eneo jingine ni mawasiliano ya simi na kuahidi kuwa wataanza kujadili masuala ya mnara wa simu .

Anaahidi watakwenda kujadiliana ili fedha zielekezwe kwenye maeneo yenye changamoto na wakibaini kuna sehemu zenye minara na huduma za mitandao miwili ama mitatu iliyopelekwa na fedha za mfuko wa mawasilino watalazimika kuihamishia sehemu ambazo hazina huduma hiyo.

"Huwezi mtu unatoka Nangurukuru unakwenda Liawale katikati hakuna mawasiliano hivi gari likapata shida huku unamuona simba au tembo huna mawasiliano ni shida ni lazima la simu tulifanyie kazi,"

**ELIMU NI TATIZO LINDI**

Chongolo anasema elimu kwa mtoto wa kike hasa Lindi ni changamoto kubwa. Ukiangalia takwimu hata ndoa za utotoni zipo juu kwa sababu mila zinachangia na wale waliopewa dhamana ya kusimamia sheria wanalegeza baadhi ya mambo.

"Ni lazima kuchukua hatua dhidi ya watu wanaoleta mchezo kwa watoto wa kike kupata elimu ushahidi unaonyesha watoto wa kike huku wana uwezo mkubwa sana tuwasaidie wautumie kwa ajili ya tija ya nchi yetu na tija za familia zao badala ya kuwapeleka kwenye ndoa za haraka ambazo hazina faida kazeni kamba tusilegezi," anasema Chongolo.

Anasema jambo hilo si la kubembelezana ni lazima wawe wakali kwa sababu wazazi ni sehemu ya hiyo michezo ya ovyo na kusababisha wanakosa haki zao.

Anafafanua kuna tatizo la miundombinu katika utoaji wa elimu kwa kuwa madarasa hayatoshi katika maeneo waliyopita wamekutana na tatizo hilo.

"Mwezi uliopita tulitoa maelekezo kila halmashauri itenga bajeti ya ujenzi wa miundombinu ya elimu na mwaka huu ni mwaka wa kwanza wanahitimu darasa la saba wa elimu bila malipo tutakuwa na mara mbili ya ongezeko la wanafunzi.

"Je, tumejipanga au tunasubiria Desemba tuzuiliwe kwenda likizo kwa ajili ya jambo ambalo hatujajipanga mapema ni lazima tujielekeze huko," anasema Chongolo.

Anawaambia jambo hilo linahitaji mambo mawili robo tatu ya fedha ya kwanza ipewe kipaumbele kwenye kutekeleza miradi ya miundombinu ya elimu na kabla ya Desemba waanze kufanya kazi ili utekelezaji usiwe zimamoto.

"Hili jambo sio la zimamoto takwimu zipo, matokeo yapo ni jambo lipo wazi wanajua inapofika Januari darasa la awali, kidato cha kwanza kuna ongezeko, tunataka waanze kutengeneza miundombinu itakayokidhi uhitaji wa wanafunzi," anasema Chongolo.

**CHANGAMOTO KIUCHUMI**

Chongola anashangaa mkoa wa Lindi unazalisha chumvi nyingi, lakini soko hakuna na baadhi wanadai kuna ujanja wa kukwamisha biashara hiyo kwa sababu kuna watu wanaagiza chumvi nje na kuisambaza.

Anasema wapo wataalamu wa serikali waliopewa dhamana wanatoa vibali kwa njia za ujanja ujanja jambo ambalo atalishughulikia.

"Ofisa madini wa Lindi yupo katika huu mkutano? Anauliza. Hayupo, hawa maofisa wanaonekana ni wakubwa hawawezi kuja vikao vidogo. Ofisa madini wa hapa hatoi kibali kinatolewa na ofisa mwenzake wa mkoa mwingine. Huu ni uhuni nitazungumza na Waziri apige marufuku utoaji wa vibali kama chumvi haifai basi viwanda vilivyopo vifungwe," anaahidi.

## KANSELA MSTAAFU ANGEL MARKEL;

# Mama wa kwanza kwenye wadhifa wenye nusu ya historia yake kisiasa

- Alianza 1989; mkuu nchi 2005 - 2021
- Nusu ya umri wake imeliwa na siasa

**Na Ester Mgidula**

NI tarehe za hekaheka na mashamsham tangu Jumapili iliyopita, siasa zimepamba moto kukishuhudiwa Wajerumani wanapata uongozi mpya, baada ya kushuhudiwa mchuano mkali wa kampeni hadi upigaji kura.

Vyama vya siasa, Christian Democtatic (CDU) na Social Democratic (SDP), hali kadhalika nyuma yao Chama cha Kijani kilichokuwa na mgombea kijana wa umri miaka 40 tu, Annalena Baerbock, mchuano ulikuwa mzito.

Hao wote wamekuwa katika 'piga nikupige' kuvaa kiatu cha Mama Angel Markel, ambaye kwa tiketi ya chama chake CDU-CSU, akampatia kijiti mrithi Rhine-Westphalia (60), waziri mwandamizi nchini humo tangu mwaka 2017.

Ikumbukwe kuwa huyo ndiye Kansela wa kwanza mwanamke kuongoza katika historia ya Ujerumani na katika matokeo mapya, SDP ndio imeibuka chaguo sahihi kwa Wajerumani.

Wameamua kumuweka aliyekuwa Waziri wa Fedha, Olaf Scholz, ambaye juzi mchana kura yake ameng'ara kwa asilimia 25.7, akifuatiwa na mrithi wa Mama Merkel aliyepata asilimia 24.1, vivyo hivyo, atokaye Chama cha Kijani, ana asilimia 14.8

Ni aina ya vita inayobeba sura ya kila ya waliowania kiatu cha Kansela Mama Agela Markel, msomi aliyetukuka katika fani ya Kemia), aliyelenga kurithi heshima ya umaarufu wenye matokeo uliomuweka madarakani mkuu wao wa nchi tangu mwaka 2005.

Mama huyo Mjerumani, ambaye viwango na fani yake ya darasani, nasaba zao haziko mbali sana na aliyokuwa nayo hayati Rais Dk. John Magufuli, safari yake ya miaka 32 katika siasa ameigawanya katika vipande viwili vinavyofanana.

Wakati miaka 16 ya kwanza ni tangu alipojiunga rasmi hadi kujikweza kuwania na kuupata ukuu wa nchi, miaka 16 mfululizo iliyofuata amekuwa akiiongoza nchi, hadi wiki hii anapostaafu, akiacha wasifu kuwa kiongozi mwenye msimamo mkali, msikivu na asiye na papara.

Vivyo hivyo, Kansela huyo wa Ujerumani, anadhihirisha uanasayansi wake, kwani umri alio nao leo wa miaka 67, historia yake inagawanyika katika hisabati ya vipande vikuu viwili vingine.

Hapo kuna miaka 35 ya uraiani inyozama katika makuzi kuanzia utotoni, darasani na taaluma ya usomi, huku miaka 32 mingine inaangukia siasa, mgawanyo unaotofautiana kwa miaka mitatu tu.

Angela Markel, safari yake katika siasa ilianza pale alipoweka kando majukumu ya usomi wa kisayansi na akahamia pilika za siasa.

Hapo alikuwa ni kijana tu 'mbichi' wa miaka 35 pekee alipewa jukumu la kuwa Msemaji wa Waziri Mkuu wa mwisho wa Ujerumani Mashariki wakati huo, Lotar de Maizire,

> Hapo ndipo nuru ya ukuu wa nchi ilipata nafasi, kwani katika miaka mitano iliyofuata, 2005, alijitosa katika kinayang'anyiro ndani ya chama na akapenya juu na kwenye uchaguzi mkuu, alivuka kuwa Kansela wa Ujerumani.



Kansela Mstaafu Angel Markel. **PICHA: MTANDAO.**

Baada ya miaka mitano nyota yake iling'aa zaidi, kwani chini ya uongozi wa Kansela Helmut Kohl mwaka 1994, alikwea kuwa Waziri wa Mazingira na Usalama wa Nyuklia.

Baada ya Helmut kushindwa kwenye uchaguzi wa mwaka 1998, Markel aliendelea kukiendesha chama hicho na mwaka 2000 alihamia ng'ambo wa pili akapanda hadi kuchaguliwa kuwa mwenyekiti wa chama chake - CDU.

Hapo ndipo nuru ya ukuu wa nchi ilipata nafasi, kwani katika miaka mitano iliyofuata, 2005, alijitosa katika kinayang'anyiro ndani ya chama na akapenya juu na kwenye uchaguzi mkuu, alivuka kuwa Kansela wa Ujerumani.

Hapo akaunda serikali ya pamoja na wapinzani wake wakuu chama cha SPD, kilichoipoka chama chake, ushindi safari hii.

Katika kipindi chake cha uongozi Markel anasifika kwa kuwa mtatuzi bora wa migogoro ya jamii na siasa uchumi, mfano alipoisadia Ugiriki kuiokoa thamani ya fedha Euro; kusaidia kukabili kusambaratika siasa za dunia, pia mikataba ya kimataifa ambayo Marekani ilipia kisogo.

Mama huyo mwenye historia ya miaka mitano ya ndoa kati ya 1977 hadi 1982 kutoka kwa msomi mwenza wa Fizikia, aitwaye Ulrich Markel na hakubahatika kupata mtoto.

Mume wake wa sasa (Joachim Sauer) ni Profesa wa Kemia, waliofunga ndoa mwaka 1998, ana watoto wawili wa kiume kwa mke wake wa awali. Kabla ya ndoa yao, wanatajwa walidumu katika urafiki wa siri wastani wa muongo mmoja.

Mama huyo alizaliwa mnamo Julai 17, mwaka 1954 mjini Humburg, Ujerumani Magharibi, kabla ya Ujerumani kuungana. Alitambulika kwa jina la Angela Dorothea Kasner.

Siku kadhaa baada ya kuzaliwa, yeye na mama yake, Herlind walihamia Ujerumani Mashariki, ambako baba yake, Horst Kasner alikuwa Mchungaji katika Kanisa la Kilutheri.

Akiwa shuleni, Markel alikuwa kinara na kuongoza somo la hisabati na lugha ya Kirusi. Alivuka hadi elimu ya juu katika Chuo Kikuu cha Karl Marx (Leipzig), akisomea Fizikia na Kemia kuanzia mwaka 1973 hadi 1978.

Alipokuwa mbioni kumaliza masomo, aliombwa kubaki katika shule ya uhandisi, pia jeshi la Polisi Ujerumani Mashariki, lakini alikataa, akiamini ingemrudisha nyuma kisiasa kutoka alichokitaja n "kumpa wakati mgumu wa kuwa ana mdomo kama kasuku."

Markel aliendelea na masomo ya Fizikia na Kemia, huko Berlin-Adlershof kutoka mwaka 1978 hadi 1990. Baada ya kumaliza shahada ya uzamivu katika Kemia, alijikita katika kazi ya Mwanasayansi Mtafiti, kisha akajisogeza kwenye siasa baadaye.

Markel hajabahatika kupata watoto, isipokuwa mumewe ana watoto wawili wa kiume kwa mke wake wa awali.



## ‘Viongozi wa dini iombeeni nchi amani, utulivu’

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Zainabu Chaula, amewataka viongozi wa dini kuiombea nchi iendelee kuwa na amani na utulivu.

Dk. Chaula aliyasema hayo juzi katika dua ya wanawake wa kiislamu iliyokuwa maalum kwa ajili ya kumbukumbu za kuzaliwa kwa Mtume iliyoenda sambamba na harambee ya ujenzi wa Msikiti wa Daru Mustapha, uliopo Kata ya Chang’ombe jijini hapa.

Katika harambee hiyo, Dk. Chaula alichangia Sh. milioni 1.5 na kuwaasa wanawake hao wajikite kwenye maombi ya kuliombea taifa lisiingie kwenye machafuko.

“Tuendelee kumwombea pia Rais wetu Samia Suluh Hassan aendelee kuliongoza taifa kwa amani kwani amani ndio msingi wa maisha yetu sisi pia Waziri wa hii wizara, Ashatu Kijaji anawapa salamu sana alitamani ahudhurie hafla hii, lakini kutokana na majukumu ameshindwa kufika hapa,” alisema.

Aidha, aliitaka jamii kuwa na moyo wa kutoa ili kukamilisha ujenzi wa nyumba hiyo muhimu kwenye maisha yao.

Awali, akisoma risala ya wanawake hao, Yusra Mcharo, alisema wanakabiliwa na ukosefu wa majengo ya kusali, hivyo kukamilika kwa ujenzi wa msikiti huo utatatua tatizo hilo.

Alisema pia kuna kituo cha kulea watoto katika eneo hilo ambapo kwa sasa kuna wanafunzi 375 na wamekuwa wakisoma katika mazingira magumu kutokana na uwapo wa uhaba wa vyumba vya madarasa.

**“Tuendelee kumwombea pia Rais wetu Samia Suluh Hassan aendelee kuliongoza taifa kwa amani kwani amani ndio msingi wa maisha yetu sisi pia Waziri wa hii wizara, Ashatu Kijaji anawapa salamu sana alitamani ahudhurie hafla hii, lakini kutokana na majukumu ameshindwa kufika hapa,” alisema.**

# Sababu kasi matumizi ya zebaki yaanikwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira imesema upatikanaji holela wa zebaki umekuwa kikwazo katika kudhibiti matumizi yake nchini.

Mkurugenzi wa Mazingira wa Ofisi hiyo, Dk. Andrew Komba, aliyasema hayo alipokuwa akifunga warsha ya siku mbili kwa waandishi wa habari kuhusu Mkataba wa Minamata na Mpango kazi wa kupunguza matumizi ya zebaki kwa wachimbaji hao iliyofanyika jijini hapa.

“Kumekuwapo na upatikanaji holela wa zebaki ambao umekuwa ukichangia ugumu katika kudhibiti matumizi ya kemikali hii ya zebaki,” alisema.

Aidha, alisema serikali imeweka miongozo na sheria za kudhibiti matumizi yasiyo sahihi ya zebaki, lakini upatikanaji holela wa kemikali hiyo imekuwa ni kikwazo kwenye kudhibiti.

“Haya matumizi yasiyo sahihi ya zebaki yamekuwa na madhara makubwa kwa afya ya binadamu na mazingira ambayo yanadumu kwa muda mrefu na vizazi kwa vizazi,” alisema.

Komba alisema serikali imekuwa ikifanya juhudi za kudhibiti matumizi holela ya zebaki ikiwamo kuweka teknolojia mbadala katika uchenjuaji dhahabu. Kwa upande wake, Mhandisi wa Mazingira kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Kamkuru Maganya, alitaja mikakati tisa ya kupunguza na kuondosha matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo.

Alisema mikakati hiyo ni pamoja na kuondosha mbinu zisizofaa ikiwa ni pamoja na uchomaji holela wa dhahabu na uchenjuaji wa marudio yenye zebaki kwa kutumia sayanaidi kunachangia zaidi uchafuzi wa mazingira.

“Shughuli mahsusi za kuondosha mbinu zisizofaa kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu zinalenga kupunguza matumizi holela ya zebaki na kuelimisha wachimbaji wadogo na jamii kwa ujumla kuhusu madhara ya zebaki na hapa tunaandaa na kutekeleza mpango wa kukuza uelewa na kutoa mafunzo kuhusu mbinu bora za udhibiti wa zebaki wakati wa uchenjuaji,” alisema.

Maganya alitaja mkakati mwingine ni tathmini ya hali halisi ya matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo ambapo itaanzishwa na kuendeshwa kanzidata za kisekta zenye taarifa za zebaki zinazohusiana na sekta ya afya, mazingira, madini na ajira.

“Mkakati mwingine ni kurasimisha sekta ya wachimbaji wadogo wa dhahabu ambapo hapa yatafanyika mambo mbalimbali ikiwamo kuandaa na kufanya mapitio na kusimamia utekelezaji wa sheria zinazosimamia na kudhibiti zebaki,” alisema.

Aidha, alisema kuna mkakati wa kupunguza uchafuzi wa mazingira utokanao na zebaki kwenye hewa, ardhi na maji ambapo wataimarisha utekelezaji na uzingatiaji wa sheria za usimamizi wa mazingira na mipango ya matumizi ya ardhi.

Mtaalamu huyo alisema pia watasimamia biashara ya zebaki, kushirikisha wadau katika kutekeleza mpango kazi, kudhibiti na kukabiliana na madhara ya zebaki kwa afya ya binadamu, kudhibiti athari za zebaki kwa makundi yaliyo hatarini hususan watoto na wanawake wenye umri wa kuzaa na kuelimisha wachimbaji wadogo wa dhahabu.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, akiwasilisha mada kwenye mkutano mkuu maalumu wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa (ALAT), jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Familia wenye ulemavu zaombwa ushirikiano wakati wa sensa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Maridhiano Mkoa wa Dodoma, Lucas Chande, ameziomba familia zinazoishi na watu wenye ulemavu kutoa ushirikiano kwa serikali wakati wa sensa ya watu na makazi itakayofanyika Agosti mwakani.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Chande, alisema kuwa zikitolewa taarifa hizo kwa usahihi kwa serikali itawatambua na kurahisisha kwenye mipango ya maendeleo.

“Baadhi ya familia zenye watu wenye ulemavu wana tabia ya kuwaficha kitendo ambacho ni cha ukatili kwa kuwa wao pia wana haki na wajibu mkubwa wa kuandikishwa kwenye zoezi hili muhimu kwa taifa letu,” alisema.

Chande alisema familia zenye wenye ulemavu wakiwaficha watasababisha serikala kuwa na mzigo katika mipango yake ya maendeleo.

Pamoja na hayo, aliomba kaya kutoa takwimu zilizo sahihi kwa maafisa ambao watakaowajibika na zoezi la sensa ili kufanikiwa kwa wakati na kufikia malengo yake yaliyopangwa.

Pia aliwaomba viongozi wa madhehebu ya dini kusaidia kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa sensa.

“Hili zoezi lisihusishwe na imani za kidini wala itikadi za siasa wananchi wahamasishwe kwa kupewa elimu ili washiriki ipasavyo,” alisema.

Alisema viongozi wa madhehebu ya dini wana nafasi kubwa ya kuelimisha kupitia nyumba zao za ibada ili kufanya sensa ifanikiwe.

“Watanzania tuanze maombi mapema ya kumwomba Mungu kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika 2025 na kuombea amani na uchumi wa nchi yetu badala ya kusubiri mpaka muda ukaribie,” alisema.





# Mgogoro KKKT Konde waingia sura mpya

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MGOGORO wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Konde umeingia sura mpya baada ya maaskofu wastaafu wa kanisa hilo kutoka dayosisi nne, kubariki hatua za kuhamisha makao makuu wa dayosisi hiyo kutoka mjini Tukuyu kwenda Halmashauri ya Jiji la Mbeya wakidai kuwa taratibu zote zilifuatwa.

Wakizungumza na Waandishi wa habari kwenye makao makuu ya dayosisi hiyo jijini Mbeya jana, maaskofu hao walisema wamejiridhisha na uamuzi wa kuhamisha makao makuu kwa sababu taratibu zote muhimu zilifuatwa kwa kuzingatia sheria na taratibu za dayosisi hiyo.

Askofu mstaafu wa Dayosisi ya Kusini (Njombe), Isaya Mengele, alisema uamuzi wa kuhamisha makao yalizingatia uamuzi ya vikao mbalimbali ukiwamo mkutano mkuu ulioketi mwezi Julai mwaka huu na kubariki makao makuu kuhamishwa.

"Kwa kuzingatia kanuni na taratibu za Dayosisi ya Konde, tunabariki uamuzi wa kuhamisha makao kuja Mbeya mjini kwa sababu ni eneo la katikati na makanisa yote ni rahisi kufika hapa kupata huduma," alisema Askofu Mengele.

Alisema mgogoro huo wa kuhamisha makao makuu ya Dayosisi umeleta majeraha ya kisaikolojia kwa sababu ni maneno mengi ya kejeli na kifedhuli yametolewa hali iliyosababisha chuki miongoni mwa waumini, wachungaji na maaskofu.

Baada ya kueleza msimamo wao kubariki kuhamisha makao makuu ya dayosisi kutoka Tukuyu kuja Mbeya mjini, aliwashauri viongozi wote wa dayosisi kumaliza tofauti zao na kuendelea kuhubiri injili.

Kwa upande wake Askofu mstaafu wa Dayosisi ya Kusini Magharibi Matamba, Job Mbwilo, alisema mwenye uamuzi wa kutengua ni dayosisi yenyewe na sio mtu mwingine nje ya dayosisi hiyo.

Alisema kwa vile uamuzi huo ni makubaliano yaliyoafikiwa kwenye mkutano mkuu kila jambo litakwenda kwa mujibu wa kanuni na sheria.

Kwa upande wake Askofu wa Kanisa la KKKT, Dayosisi ya Konde, Dk. Edward Mwaikali, alisema hajawahi pokea mezani kwake hoja za kupinga dayosisi hiyo.

Alisema hakuna taarifa rasmi iliyomfikia kuhusu kupinga uamuzi huo badala yake baadhi ya wachungaji na waumini wanapinga uamuzi huo kwa maneno ya chini chini ambayo kimsingi hayana afya.

Aliwataka waumini wa kanisa hilo kuungana kwa pamoja kuhubiri neno la Mungu badala ya kuendelea na malumbano ambayo hayana tija kwa ustawi wa kutangaza habari njema za wokovu.



Wajumbe wa kamati ya afya ya msingi ya Jiji la Mbeya, wakifuatilia semina ya uzinduzi wa mpango harakishi na shirikishi wa chanjo ya ugonjwa wa Corona (UVIKO 19), jijini humo juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wahukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa mauaji

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania, Kanda ya Mbeya, imewahukumu kunyongwa hadi kufa watu wawili wakazi wa Mbarali mkoani Mbeya baada ya kukutwa na hatia ya mauaji ya mama mkwe marehemu Zaituni Samsoni (57) ili kupata utajiri.

Waliohukumiwa kunyongwa ni Isaya Chungu (37), mkazi wa Udindilwa na James Mwaikuka (32), mkazi wa Ruiwa ambao walikuwa wakishtakiwa na Jamhuri kwa tuhuma za mauaji ya mama mkwe wa mshtakiwa wa kwanza marehemu Zaituni Samson, kosa ambalo kisheria ni kinyume na kifungu namba 196 & 197 cha Sheria ya Makosa ya Jinai sura ya 16 kilichofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

Akisoma hukumu hiyo, Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya, James Karayemaha, alisema upande wa mashtaka umethibitisha bila kuacha shaka yoyote washtakiwa wote wawili kwa pamoja kumuua mtu huyo mnamo Februari 16, 2013 huko katika kijiji cha Udindilwa, wilayani Mbarali licha ya washtakiwa kukana kutenda kosa hilo.

Akirejea sehemu ya ushahidi wa Jamhuri uliotolewa mahakamani hapo, Jaji Karayemaha alisema kwa mujibu wa maelezo ya mashahidi mbalimbali na vielelezo wakiwamo maofisa wa polisi na wataalamu wa afya ni wazi kwamba mama huyo alifariki dunia kutokana na kukabwa shingo na baadaye kumjeruhi na kumsababishia pia kuvuja damu nyingi.

Imeelezwa mshtakiwa wa kwanza ambaye ni mkwe wa marehemu aliungana na mwenzake kumuua mtu huyo ili waibe dawa kwa kuwa inadaiwa alikuwa akiuza dawa za kuwezesha mtu kutajirika na walitaka kupata dawa hizo ili kwenda kuzitumia kwenye shughuli za machimbo wilayani Chunya.

Mshtakiwa wa kwanza Isaya Chungu alikuwa akiwakilishwa mbele ya mahakama hiyo na Wakili Alfred Chapa na Wakili Stewart Ngwale, alikuwa akimwakilisha mshtakiwa wa Pili James Mwaikuka.

Waendesha mashtaka wa serikali kwenye shauri hilo wakiwa ni wakili Davice Msanga na mwenzake Xaveria Makombe, waliiomba mahakama kutoa adhabu stahiki ili iwe fundisho kwa washtakiwa na watu wengine.

Alifafanua kuwa kutokana na kukithiri kwa matukio mbalimbali ya uhalifu utokanao na imani za kishirikina hata kugharimu maisha ya watu kutokana na kuendekeza imani potofu za kuamini dawa za kienyeji kwamba zinaweza kuwasaidia kupata utajiri hata kuathiri maisha ya watu akiwamo marehemu.

Jaji aliyesikiliza shauri hilo, James Karayemaha aliamuru washtakiwa hao wawili kwenda kunyongwa hadi kufa kutokana na kuthibitishwa kwa kesi hiyo ya mauaji ya mama mkwe na kueleza kwamba wasioridhika na uamuzi wa mahakama hiyo wana haki ya kukata rufani Mahakama ya Rufani Tanzania.

## Watumishi Idara ya Afya watakiwa kupata chanjo

**Na Grace Mwakalinga,** SUMBAWANGA

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Joseph Mkirikiti, amewasisitiza watumishi wote wa Idara ya Afya mkoani humo, kupata chanjo hiyo ili wananchi wawe na imani ya usalama wa chanjo ya ugonjwa wa Corona (UVIKO-19) inayotolewa na baadhi yao kuacha kutoa taarifa za upotoshaji.

Mkirikiti alitoa kauli hiyo juzi baada ya Mkuu wa Wilaya Kalambo, Tano Mwera kudai baadhi ya watumishi wake hawamuungi mkono kwenye kampeni ya kuhamasisha wananchi kupata chanjo ya UVIKO-19.

"Serikali inafanya jitahada za kuwapatia wananchi chanjo kukabiliana na ugonjwa wa UVIKO-19, lakini watu wachache wanatoa kauli za kukatisha tamaa, nasema hili halikubaliki 'kitaumana' tutawashughulikia, neno hiari lisitumike vibaya hatutakubali kuona baadhi yetu wanawaambukiza wenzao kisa hawajapata chanjo kila mwananchi mwenye sifa ya kupata chanjo atachanjwa," alisema Mkirikiti.

Aliwaagiza wakuu wa vyombo vya usalama hususani Jeshi la Kujenga Taifa kabla ya vijana wanaopata mafunzo ya kuhitimu wapate chanjo ya corona na Jeshi la Polisi kuhakikisha maeneo yote ya biashara kama vile gulio, wafanyabiashara wanaoingia na kutoka wanapata chanjo.

Alimtaka Mganga Mkuu wa mkoa huo, Dk. Boniface Kasululu, kufungua vituo vya utoaji chanjo kwenye maeneo mbalimbali ili kuwapunguzia gharama wananchi kufuata huduma hiyo kwenye vituo vya afya vilivyokuwa vimepangwa awali.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Dk. Boniface Kasululu, alisema mkoa ulipokea chanjo 20,000 za UVIKO-19 na hadi sasa ni watu 1,300 pekee sawa na asilimia 15 waliochanjwa.

Alibainisha kuwa Wilaya ya Nkasi jumla ya chanjo 48,000 zilitolewa na watu 542 ndio walipata chanjo hiyo, Kalambo jumla ya chanjo 2,400 zilitolewa na wananchi waliopata ni watu 233.

Alisema idadi ya waliochanjwa ni ndogo kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo imani potofu kwamba chanjo hizo zinaathari kiafya jambo ambalo sio kweli.

Mkuu wa Wilaya ya Kalambo, Tano Mwera, alisema imani potofu kwa baadhi ya wakazi wa eneo hilo imechangia zoezi la chanjo kutofanikiwa kama ilivyokusudiwa huku akiwalalamikia watendaji wa kata, vijiji na wenyeviti kutomuunga mkono katika jitahada za kuhamasisha utaoji wa chanjo hiyo.

Kwa upande wake, Chifu Charles Katata kutoka himaya ya Nkasi Milanzi ambaye pia Mwenyekiti wa Umoja wa Machifu mkoani Rukwa, alisema yeye ni miongoni mwa watu waliopata chanjo siku za mwanzo na aliwatoa hofu kuwa hakuna madhara yoyote aliyoyapata.

Alisema kwa imani zao walijiridhisha na ubora na usalama wa chanjo hizo na aliwahamasisha na wengine kuchanjwa ili kuimarisha kinga za mwili katika kupambana na ugonjwa huo.

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Ziwa Tanganyika ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Amani mkoa, Ambele Mwaipopo alisema baadhi ya waumini waliingiwa na hofu ya chanjo hiyo baada ya kudanganywa kuwa ni alama za 666 inayozungumwa kwenye Biblia jambo ambalo alikanusha.

Alisema kwa umuhimu wa chanjo hiyo yeye ni miongoni mwa waliopata na kwamba amekuwa na utaratibu wa kuhamasisha waumini wake wote kuchanjwa.

Ofisa Programu wa Mpango wa Taifa wa Chanjo kutoka Wizara ya Afya, Zainabu Nyamungumi alisema hali ya utaoji chanjo wilayani humo hairidhishi na kuwasisitiza viongozi hususani watumishi wa Idara ya Afya, kuongeza kasi ya utoaji elimu kwa wananchi ili kumaliza dozi zilizobakia.



# Mradi wafanikiwa kurejesha watoto 2,500 shuleni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kupitia mradi wa kuwarejesha shule wanafunzi watoro unaotekelezwa na Shirika la Elimu kwa wote la Qatar (EAC), imefanikiwa kuwarejesha shule watoto 2,500 kati ya watoto 35,732 waliotoroka shule za Unguja na Pemba.

Wanafunzi hao ambao wengi wao walitoroka shule wakiwa katika elimu ya msingi na kujihusisha na biashara, uvuvi na ufugaji.

Akizungumza na waandishi wa habari katika shule mbalimbali za Unguja, Mratibu wa mradi wa kuwarudisha watoto shuleni, Mzee Shirazi alisema watoto hao walikuwa katika hali hatarishi katika jamii.

Alisema wamefanikiwa kurudi shule baada ya juhudi za pamoja zilizofanywa na viongozi wa shehia na wazazi wa watoto hao.

Alisema utafiti uliofanywa umebaini kwamba watoto wengi walioacha shule ni wale wanaoishi katika mazingira magumu na kwamba fedha zilizotengwa katika mradi huo zitahudumia watu wanaoishi katika mazingira magumu.

"Tumefanikiwa kuwarudisha shule jumla ya watoto 2,500 kwa upande wa Unguja ambapo juhudi zaidi zinahitajika katika kuhakikisha tunawasaidia kiuchumi ikiwamo kuwapatia sare za shule na madaftari," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Mipango Sera na Utafiti wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Khalid Masoud Waziri, alisema utafiti uliofanywa umebaini kwamba watoto wengi wameacha shule na kujiingiza katika ajira ikiwamo za uvuvi na kugonga kokoto.

Alisema kuwa maeneo ya mwambao wa pwani yameathirika zaidi ambapo watoto hujikita katika kazi za kuvua samaki pamoja na kutembeza watalii.

"Utafiti wetu umebaini kwamba maeneo yaliyopakana na bahari ikiwamo Mkoa wa Kaskazini Unguja na yale yaliyoshamiri maendeleo ya sekta ya utalii yameathirika vibaya watoto wengi wametoroka shule huku wakizurura ovyo mitaani," alisema.

# Sensa vyombo vya usafiri majini, uvuvi Oktoba Mosi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Uwakala wa Meli Tanzania linatarajia kufanya sensa ya vyombo vidogo vya usafiri wa maji ikiwa ni pamoja na vyombo vya uvuvi vyote nchini itakayofanyika Oktoba Mosi hadi 30.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika Mamlaka ya Usafiri baharini Zanzibar, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), Kaimu Abdi Mkeyenge, alisema sensa hiyo itafanyika katika maeneo yote yenye vyombo vidogo vya usafiri wa majini na uvuvi katika mikoa yote ya mwambao wa Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na maeneo mengine ya maji yanayotumika katika usafiri wa majini na uvuvi.

Alisema vyombo vya usafiri wa majini hutumika kwa shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusafirisha abiria, mizigo, uvuvi, utalii na matumizi mengine katika maeneo ya maji nchini.

"Vyombo vya usafiri wa majini vina mchango mkubwa kiuchumi na pia huwezesha shughuli mbalimbali za kijamii," alisema.

Alisema sensa hiyo itawezesha kupata faida ya kuvitambua vyombo vidogo vya usafiri wa majini vilivyopo na maeneo ambayo vinatoa huduma ya usafiri au kufanya shughuli za uvuvi.

Alisema pia kutasaidia kutengeneza kanzidata ya vyombo vidogo vya usafiri majini na uvuvi Tanzania Bara ambapo kanzidata hiyo itatumika katika kuboresha sera, mipango, utekelezaji na usimamizi wa sheria, kanuni na maagizo ya kiudhibiti kuhusu ulinzi, usalama wa usafiri wa majini na kuzuia uchafuzi wa mazingira.

"Sensa hii ina manufaa makubwa kwa nchi kwa kuwa itatupatia taarifa sahihi kuhusu vyombo vidogo vya usafiri wa majini na uvuvi na hivyo kuwezesha utungwaji wa sera na mipango sahihi kuhusu vyombo hivi kwa kutumia takwimu sahihi itakayotengeneza mchango wa uchumi wa rasilimali za maji katika kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi, kutengeneza fursa za ajira na kupunguza umaskini nchini," alisema.

Alisema sensa hiyo pia itasaidia katika ufuatiliaji wa matokeo ya utekelezaji wa sera au mipango mbalimbali, kuwezesha ufanyaji wa tafiti mbalimbali, ufanyaji wa uamuzi wa uwekezaji na biashara kuhusu vyombo vidogo na usafiri wa majini na uvuvi kwa ujumla.

Aliwataka wamiliki wa vyombo vidogo vya majini na wananchi kujitokeza na kutoa ushirikiano kwa wadadisi watakaopita katika maeneo yao ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa sahihi na kufanikisha sensa hiyo ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya nchi.

Alisema katika sensa hiyo hakutakuwa na gharama yoyote itakayotozwa na kuwataka wamiliki wa vyombo vya majini ambavyo havijaruhusiwa kubeba abiria kutobeba kwa sababu kufanya hivyo ni kuhatarisha maisha.



Baadhi ya wanafunzi waliokuwa watoro katika shule ya Fukuchani, Kaskazini Unguja, wakiwa darasani shuleni hapo jana, baada ya kurejeshwa kupitia mradi wa kuwarejesha shule wanafunzi watoro unaoendeshwa na Wizara ya Elimu. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Masheha watakiwa kukamilisha usajili vyeti vya kuzaliwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MASHEHA wametakiwa kukamilisha mchakato wa kuwasajili watoto katika shehia zao kwa ajili ya upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa na kuondoa tatizo linalojitokeza la kuanza shule elimu ya maandalizi na msingi bila vyeti hivyo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaaa na Idara Maalumu SMZ, Masoud Ali Mohamed, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na masheha kuhusu vyeti hivyo.

Alisema yapo malalamiko ya watoto wengi kushindwa kusajiliwa na kuorodheshwa kupata vyeti vya kuzaliwa.

Pia, alisema ni aibu katika karne hii kuona mtoto anaanza shule ya maandalizi hadi msingi kwa zaidi ya miaka miwili akiwa hana cheti cha kuzaliwa.

"Inasikitisha sana kuona mtoto anamaliza elimu kidato cha nne akiwa hana cheti cha kuzaliwa matokeo yake anashindwa kujiendeleza kwa kupata elimu ya juu huku kigezo kikubwa cheti cha kuzaliwa," alisema.

Aliwataka watendaji wa wakala wa usajili wa matukio ya kijamii kuyatembelea maeneo yenye changamoto kubwa za matatizo ya vyeti vya kuzaliwa ikiwamo kisiwa cha Tumbatu na majimbo mengine ya Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Ussi Khamis Nyange, Sheha wa Gomani Tumbatu, Mkoa wa Kaskazini Unguja, amekiri kuwapo kwa changamoto kubwa za ukosefu wa vyeti vya kuzaliwa tataizo ambalo limechangiwa na jamii kutoona umuhimu wa cheti hicho.

Alisema mtoto anazaliwa, lakini inachukuwa muda wa mwaka mmoja au zaidi ndipo mzazi anapoanza kutafuta cheti cha kuzaliwa wakati muda umekuwa mrefu huku mtoto akiwa katika harakati za kuanza masomo.

"Wakati fulani tatizo la ukosefu wa vyeti vya kuzaliwa vya watoto unachangiwa na wazazi wenyewe kushindwa kufuatilia taratibu za kupata vyeti," alisema.

Naye Ofisa Tawala wilaya ndogo Tumbatu, Khatib Habib, alisema utaratibu wa zamani wa kufanya usajili wa vyeti vya kuzaliwa katika wilaya ndogo wa Tumbatu, ulisaidia kuharakisha zoezi hilo na kupunguza urasimu wa upatikanaji wa vyeti hivyo.

"Nadhani wakati umefika wa kurudisha utaratibu wa zamani wa kukamilisha mchakato wa kupata vyeti vya kuzaliwa katika eneo moja la wilaya ndogo ya Tumbatu na kuondoa urasimu wa kuvuka bahari kwenda eneo jingine," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA ENTEPRISES FINANCE LIMITED (EFL). KWA MAWASILIANO ZAIDI **TUPIGIE:0677 111 333 AU 0758 112 332**

NYUMBA INAUZWA
Ipo Kijitonyama Ali maua"A" inavyumba 3 vya kulala, Sebule, kuna sehemu ya garage, frame ya duka. Ukubwa wa kiwanja ni 700 Sqm. Eneo lipo pembezoni mwa barabara ya lami. Bei maelewano. Mawasiliano: 0782 574 669 au 0621 879 477.

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ALFRED BEATI NGOWI** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari , Yenye namba za usajili **T 254AFM** .Mistubishi Chassis namba **V434005835,** Engine namba **6G72TH5664** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . Polisi Taarifa : **KIL/MOS/RB/465820/2021**

116480702

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 14 OF 2021**
**In the Matter of the Estate of the Late GILBERT LUCAS MFINANGA**

By 1. VICTOR GILBERT MFINANGA
2. MARY DANIEL MSANGI

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the **21 day of OCTOBER 2021**
Dated at **MOROGORO** this...... .............22 day of 9 ...........................2021

RESIDENT MAGISTRATE

116480802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI DAR ES SALAAM KISUTU**
**EXECUTION NO.74/2019**
(Shauri la Madai No. 177/2018)
**AKIBA COMMERCIAL BANK .................................. MDAI**
**DHIDI YA**
**DEODATUS PANCRAS MATEMU ................................ MDAIWA**

**KWA:**
**DEODATUS PANCRAS MATEMU -** POPOTE MLIPO

**KUITWA SHAURINI**
Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake ambayo maelezo ya Mdai yameelezwa katika nakala ya madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo Mnahitajiwa/Unahitajiwa kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa, siku ya tarehe **18** Mwezi **Oktoba,** 2021 Saa **7.00** mchana mbele ya **Mhe. Isaya, SRM.**

**ANGALIA:**
Kama hamtahudhuria/hautahudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama itaweza kutoa hukumu bila ya uwepo wako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama hii leo tarehe 02 Mwezi Septemba, 2021.

**HAKIMU MKAZI/ MKUU/MWANDAMIZI**
**DAR ES SALAAM – KISUTU**

116480902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI DAR ES SALAAM KISUTU**
**EXECUTION NO.94/2019**
(Shauri la Madai No. 174/2018)
**AKIBA COMMERCIAL BANK .................................. MDAI**
**DHIDI YA**
**STANLEY NYIGANA MARO ................................ MDAIWA**

**KWA:**
**STANLEY NYIGANA MARO -** POPOTE MLIPO

**KUITWA SHAURINI**
Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake ambayo maelezo ya Mdai yameelezwa katika nakala ya madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo Mnahitajiwa/Unahitajiwa kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa, siku ya tarehe **18** Mwezi **Oktoba,** 2021 Saa **7.00** mchana mbele ya **Mhe. Isaya, SRM.**

**ANGALIA:**
Kama hamtahudhuria/hautahudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama itaweza kutoa hukumu bila ya uwepo wako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama hii leo tarehe 08 Mwezi Agosti, 2021.

**HAKIMU MKAZI/ MKUU/MWANDAMIZI**
**DAR ES SALAAM – KISUTU**

116480902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**KAGERA LILILOPO BUKOBA**
**MAOMBI MADOGO NA. 222/2021**
**YUDES EMMANUEL................MWENYE TUZO**
**DHIDI YA**
**EVARISTA EMMANUEL ......MSHINDWA HUKUMU**
**KWA: EVARISTA EMMANUEL**
**(POPOTE PALE ULIPO)**

Unaarifiwa kuwa Maombi Madogo **Na. 222/2021** yamepangwa kutajwa **tarehe 08/11/2021** mbele ya Mwenyekiti wa Baraza R. Mtei saa 2:00 asubuhi.
Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.

**AMRI** hii imetolewa kwa mkono wangu na **MUHURI** wa Baraza hili leo **tarehe 10/09/2021.**

..............................................
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
BUKOBA

116481102

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**FORM 11**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya Mwanzo MAKANG'WA SLP 923 DODOMA.**
**Usimamizi wa Mirathi No. 10, 2021.**
**Ombi la ELIAZAR EMANUEL KILONZO Kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu NASIKIWA WEMAEL ANDREA ALIYEISHI MLOWA BARABARANI W/CHAMWINO.**

**Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA KATIKA MIRATHI No 10/2021**
Watu wote wanadaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo **TAREHE 01/10/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upoo mahakamani waweza kukaguliwa
**Tarehe 24/09/2021.**

Tarehe 24/09/2021.

116481202

## KUPOTELEWA NA CHETI



**GEOFREY NEHEMIA MWASHIHAVA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA **S.3736/0056** KILICHOTOLEWA MWAKA **2018** NA BARAZA LA MITIHANI TANZANIA[NECTA] KUPITIA SHULE YA SEKONDARI DESTINY. YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/364066/2021**

116481302

## KUPOTELEWA NA CHETI



**STANSLAUS P. KIRIA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.2380/0092** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **OKAONI SEKONDARI** mwaka **2009.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi: **DAR/MBU/RB/467462/2021.**

116481502

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**AMBIKILE NDANILA MWASAPILE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA LANDCRUISER** yenye namba za usajili **T. 873 BUD,** Chasisi namba **JTELB71J30101006** Engine namba **1HZ20341486,** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi Taarifa: **ARU/PIY/RB/174750/2021.** Pia **AMBIKILE NDANILA MWASAPILE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MITSUBISHI FUSO** yenye namba za usajili **T.415 CES,** Chasisi namba **FK71GC750055,** Engine namba **6M61008784** kwa yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi Taarifa: **ARU/PIY/RB/174723/2021.**

116481802

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
IDARA YA UHAMIAJI

**TANGAZO LA OMBI LA URAIA**



**BW. PATRICIA AYUMA OPATI**

Hii ni kwa taarifa kwamba: **PATRICIA AYUMA OPATI S.L.P 6500, DAR ES SALAAM.**
Mwenye picha hapo juu, anaomba uraia wa Tanzania kwa Mhe. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Utaifa wake wa sasa ni MKENYA. Nchi atokayo ni KENYA. Shughuli zake ni DAKTARI na anwani yake ni S.L.P…Dar es salaam.
Yupo hapa nchini tangu 2012. Kwa yeyote mwenye taarifa/sababu za kwanini mwombaji asipewe Uraia wa Tanzania, atume taarifa kwa maandishi kwa

Kny: KAMISHNA JENERALI WA UHAMIAJI
Kamishna Jenerali wa Uhamiaji
S.L.P 512, Dar es salaam. Kumb Na. DN.
…………….......................................

116481702

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**OSCAR BUNDALLAH HOSSEA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina **TOYOTA LANDCRUISER** yenye namba za usajili T 860 BDK. Chassis no. **JTECB09J903022091**.Engine No.1HZ0479799 Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/460527/2021**

116482502

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO MJINI**
**Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na.42/2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MOHAMED OMARY SHAKHRY wa CHINANGALI DODOMA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SOPHIA ALLY KAWANGO**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama ya mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 12/10/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 21/09/2021.

116482402

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

116480302

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## TANGAZO

# TCB YAANDAA KONGAMANO LA PILI LA WANAWAKE NA BIASHARA JIJINI MBEYA



*Mgeni rasmi kwenye Kongamano la Pili la Wanawake na Biashara lililoandaliwa na Benki ya Biashara Tanzania (TCB) Ijumaa iliyopita jijini Mbeya, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Dkt. Tulia Ackson (kushoto), akicheza pamoja na kikundi cha ngoma mara baada ya kuwasili kwenye warsha hiyo ya kuwawezesha akinamama kiuchumi iliyofanyika katika Ukumbi wa Dhamira uliopo kwenye Hoteli ya Modern Highland.*




*Naibu Spika Dkt. Tulia Ackson (kushoto) akiteta jambo na Mkurugenzi Mkuu wa TCB, Bw. Sabasaba Moshingi, kabla ya yakuzindua rasmi Kongamano la Pili la Wanawake na Biashara wiki iliyopita. Kongamano la ufunguzi na la kwanza lilifanyika mwanzoni mwa mwezi huu jijini Dodoma.*




*Mkurugezi Mkuu wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Bw. Sabasaba Moshingi, akisisitiza jambo wakati wa Kongamano la Wanawake na Biashara la Mbeya liliohudhuriwa na washiriki zaidi ya 250 na kuambatana na maonyesho ya akinamama wajasiriamali wateja wa benki hiyo kongwe kuliko zote nchini.*




*Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Dkt. Tulia Ackson (wa pili kushoto mbele), katika picha ya pamoja na viongozi wakuu wa TCB na maofisa waandamizi wa benki hiyo ambayo imejipanga kuwakwamua wanawake kiuchumi kupitia suluhishi zake za kifedha.*




*Miongoni mwa viongozi wa serikali walioshiriki kwenye warsha hiyo ni Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dkt. Rashid Chuachua, aliyesisitiza umuhimu wa akinamama wajasiriamali kuelimishwa jinsi ya kufanya biashara zenye tija kwa manufaa yao binafsi na maendeleo ya taifa kwa ujumla.*



*Baadhi ya akinamama wajasiriamali wa Mbeya walioshiriki kwenye Kongamano la Wanawake na Biashara la TCB wakifuatilia kwa makini mafunzo mbalimbali kutoka kwa wachokoza mada wa warsha hiyo ambao wote walikuwa wafanyakazi wanawake wa benki hiyo.*

216482701

HABARI MICHEZO

# AZAM YAJISAHAULISHA YA COASTAL, YAGEUKIA POLISI

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

BAADA ya kushindwa kuvunja rekodi ya kupata matokeo chanya, kwenye Uwanja wa Mkwakwani, jijini Tanga, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amesema sasa wanasonga mbele katika kuelekeza nguvu zao, kwenye mchezo ujao, dhidi ya Polisi Tanzania.

Kikosi cha Azam FC juzi kiliishia kulazimisha sare ya bao 1-1, dhidi ya Coastal Union katika Uwanja wa Mkwakwani na kushindwa kuvunja rekodi yao ya kupata pointi tatu katika dimba hilo, lililopo katikati ya Jiji la Tanga, hivyo leo kitaelekea mjini Moshi tayari kwa mchezo wao, unaofuata dhidi ya Polisi Tanzania, utakaopigwa Jumamosi wiki hii, katika Dimba la Ushirika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Bahati alisema mchezo huo dhidi ya Coastal Union, ulikuwa na ushindani mkubwa na wachezaji walipambana na kupata pointi moja, ambayo kwao ni muhimu hasa ukizingatia ni mchezo wa kwanza, kwenye ligi hiyo.

"Hatukuweza kufikia malengo yetu katika mchezo wetu, dhidi ya Coastal Union na kuondoka na pointi moja, mwisho wa mchezo huu ni mwanzo wa maandalizi ya mechi yetu ijayo, dhidi ya Polisi Tanzania," alisema.

Alisema wanafanyia kazi udhaifu wao uliyojitokeza katika mechi yao, dhidi ya Coastal Union ikwamo kuimarisha zaidi safu ya ushambuliaji, ili kutumia vema nafasi wanazotengeneza.

"Kuhusu safu ya ulinzi, tunaendelea kufanyia kazi tatizo, ambalo hata msimu uliopita tulikuwa nalo, hasa kuruhusu bao ilhali tunaongoza, hivyo tunalifanyiwa kazi kwa umakini kuhakikisha mechi zijazo makosa hayo hayajirudii.

Azam ikiwa Uwanja wa Mkwakwani, msimu wa 2018/19 iliambulia sare ya bao 1-1, kabla ya kuchapwa bao 1-0, msimu uliofuata wa 2019/20. Azam ilichapwa mabao 2-1 msimu uliopita, kwenye uwanja huo, dhidi ya Coastal Union na juzi ikiambulia tena sare ya bao 1-1.

Pia, hii ni mara ya kwanza kwa Azam kushindwa kupata ushindi, kwenye mechi ya kwanza baada ya misimu minne.

Mara ya mwisho kutoka sare, kwenye mechi ya ufunguzi ilikuwa ni Agosti 20, 2016 ikifungana bao 1-1, dhidi ya African Lyon msimu wa 2016/17.

Msimu ulifuata ilishinda bao 1-0, dhidi ya Ndanda FC, 2018/19 ikaichapa Mbeya City mabao 2-0, ikashinda bao 1-0 kwa misimu miwili iliyofuata, dhidi ya KMC na Polisi Tanzania, 2019/20 na 2020/21.

**TWENDE KAZI...**



Wachezaji wa Yanga, Fiston Mayele (kushoto) na Deus Kaseke wakiwa katika maandalizi ya mchezo wao wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Kagera Sugar, utakaopigwa, Uwanja wa Kaitaba, mjini Bukoba leo. **PICHA: YANGA**

## Harerimana ataka makali zaidi Mbeya Kwanza

**Na Saada Akida**

LICHA ya kuanza vema msimu mpya wa Ligi Kuu Bara 2021/22, Kocha Mkuu wa Mbeya Kwanza FC, Harerimana Haruna, amesema bado anahitaji kuongeza juhudi na nguvu ndani ya kikosi chake, ili kuhakikisha anaiweka timu hiyo sehemu nzuri, mwishoni mwa msimu.

Mbeya Kwanza inayoshiriki kwa mara ya kwanza Ligi Kuu msimu huu, juzi ilianza vizuri baada ya kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Mtibwa Sugar, kwenye mchezo wa ufunguzi uliopigwa Uwanja wa Mabatini mkoani Pwani.

Akizungumza na gazeti hili jana, Harerimana alisema ushindi huo wa kwanza hautampa kiburi cha kuona kikosi chake ni kamili zaidi ya kuhakikisha anaongeza juhudi na nguvu, ili kuendelea kupata matokeo chanya katika michezo iliyopo mbele yao. Alisema walikuwa na maandalizi mazuri ya msimu mpya kwa kucheza mechi 11 za kirafiki, ambazo zimewasaidia kupata muunganiko mzuri wa timu hiyo na kuweza kupambana.

"Sawa tumeshinda mbele ya wenyeji wetu, bado ni mwanzo wa ligi tunahitaji kujipanga vizuri na kufanyia kazi mapungufu yetu kuhakikisha mwisho wa msimu tunaiweka Mbeya Kwanza sehemu nzuri," alisema Harerimana.

Alisema baada ya mechi ya Mtibwa Sugar wamerejea kwao Mbeya, kujiandaa na mechi, dhidi ya ndugu zao Mbeya City, ambayo itapigwa katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine Jumapili, wiki hii.

"Kazi kubwa ni kufanyia kazi mapungufu yetu ikiwamo umakini wa safu ya ushambuliaji na mabeki, itakuwa mechi ya ushindani mkubwa, kwa sababu wote tunatoka Mbeya na kucheza katika uwanja wa nyumbani licha ya kwamba, kwenye mechi hiyo tutakuwa ugenini," alisema Harerimana.

## Morocco, Ndayiragije na siri ushindi, kichapo

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kuanza kwa ushindi kwenye Ligi Kuu Bara, Kocha Mkuu wa Namungo FC, Hemed Morocco, amesema siri ya kupata matokeo chanya ni wachezaji wake kufuata maelekezo, pia kambi nzuri waliyoiweka jijini Arusha, kujiandaa kujiandaa na msimu huu mpya wa 2021/22.

Ikiwa nyumbani katika Uwanja wa Ilulu, mkoani Lindi juzi, Namungo iliibuka na ushindi wa mabao 2-0, dhidi ya Geita Gold FC, iliyopanda Ligi Kuu msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana kuhusu mchezo huo, Morocco, mbali na kuwapongeza wachezaji wake kwa kufanya vizuri, alisema ushindi huo ni matokeo ya kambi nzuri waliyoiweka Arusha, pia kufuata maelekezo aliyowapa.

Alisema mchezo ulikuwa mgumu na wenye ushindani na kwamba licha ya Geita Gold ndiyo imepanda daraja msimu huu, lakini kikosi chake kinaundwa na wachezaji wazuri.

"Nimefurahishwa na matokeo tuliyoyapata baada ya kupata pointi tatu, ingawa mchezo ulikuwa mgumu na wenye ushindani, lakini wachezaji wangu wamefuata maelekezo yangu vizuri na ushindani huo, tutauendeleza kwa msimu huu wote," alisema Morocco huku akiwashukuru mashabiki wa timu hiyo pamoja na wadau wote wa mkoani humo, kutokana na ushirikiano mzuri waliowapa.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Geita Gold, Etienne Ndayirajige, alisema licha ya kupoteza mchezo wao wa kwanza, hakuna kilichoharibika kwa kuwa, ndiyo kwanza ligi imeanza.

Ndayirajige alisema mchezo huo ulikuwa mgumu na wenye ushindani na kwamba matokeo hayo, wanayapokea kama sehemu ya kwenda kurekebisha makosa yaliyojitokeza

"Makosa madogo madogo ambayo yamejitokeza, nimeyaona, ninakwenda kuyafanyia kazi, ili yasijirudie katika michezo mingine ya Ligi Kuu, tunaomba mashabiki wetu wasikatishwe tamaa na matokeo hayo,"alisema Ndayirajige.

Alisema wapinzani wao walipata nafasi wakazitumia hivyo kuwafanya kukubali kichapo cha mabao 2-0, wakiwa ugenini.

## ZISIKUPITE

### UNITED YAMGEUKIA PHILLIPS
KLABU ya Manchester United, imeamua kuelekeza nguvu zake kwa nyota wa Leeds United, Kalvin Phillips, mwenye umri wa miaka 25, baada ya kuachana na mipango yao ya kumtaka, Declan Rice mwenye umri wa miaka 22, kutoka West Ham. **(Star)**

### RICE KUUZWA PAUNI MIL 90
WEST Ham ina mpango wa kumuuza mlinzi wake Declan Rice, mwenye umri wa miaka 22, kwa dau la pauni milioni 90, ili iweze kumpata mrithi wake**. (Football Insider)**

### PORRO ATAKIWA REAL MADRID
REAL Madrid inafikiria kupeleka ofa, kwa ajili ya mlinzi wa pembeni wa Hispania, Pedro Porro, mwenye umri wa miaka 22, ambaye yuko kwa mkopo Sporting Lisbon akitokea klabu ya Manchester City. **(O Jogo)**

### DE LIGT, DEPAY KUPISHANA
BARCELONA bado ina nia ya kutaka kumsajili mlinzi wa Juventus na timu ya Taifa ya Uholanzi, Matthijs de Ligt, mwenye umri wa miaka 22 na iko tayari kumtoa golikipa Mjerumani, Marc-Andre ter Stegen, mwenye umri wa miaka 29 na mshambuliaji Memphis Depay (27), kama sehemu ya kukamilisha mpango huo. **(Calciomercato)**

### KASSIE AGOMBEWA EPL
LIVERPOOL na Manchester United ni miongoni mwa klabu za England zinazotajwa kumfuatilia kiungo wa Ivory Coast, Franck Kessie, mwenye umri wa miaka 24, ambaye amegoma kutia saini mkataba mpya na klabu yake ya AC Milan. **(90min)**

### ISCO, JOVIC KUTUA EVERTON
KOCHA wa Everton, Rafael Benitez, anataka kuwasajili kiungo wa Hispania, Isco mwenye umri wa miaka 29 na mshambuliaji wa Serbia, Luka Jovic mwenye umri wa miaka 23, pale Goodison Park, wakitokea Real Madrid kwa mkataba mfupi wa mkopo Januari. **(Defensa Central)**

### DAVIES ATAKIWA PALACE
KLABU ya Crystal Palace inamfuatilia kwa makini, Tom Davies, mwenye umri wa miaka 23, kutoka Everton baada ya hali ya sintofahamu ya mustakabali wa kiungo huyo wa England**. (Football Insider)**

### BARCA YAMTAKA SWEDBERG
BARCELONA inataka kumsajili kiungo kinda raia wa Sweden mwenye umri wa miaka 17, Williot Swedberg kutoka Hammarby**. (Expressen)**

### LANG TAYARI KUTUA ARSENAL
MSHAMBULIAJI wa Club Brugge, Noa Lang yuko tayari kutua Arsenal, lakini 'Washikabunduki' hao wa London wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa AC Milan, wanaomtaka pia mholanzi huyo, mwenye umri wa miaka 22**. (Voetbal24 via Mirror)**

### HAALAND AMULIKWA MADRID
MTENDAJI Mkuu wa Borussia Dortmund, Hans-Joachim Watzke, amesema Real Madrid ni klabu "inayomshawishi" Erling Haaland, mwenye umri wa miaka 21, wakati huu mshambuliaji huyo wa Norway, akiangalia mustakabali wake wa baadaye. **(AS)**

### CLEARY AGOMBEWA UJERUMANI
KLABU za Dortmund na Hoffenheim zinamfuatilia kwa karibu mshambuliaji wa England, Reyes Cleary, mwenye umri wa miaka 17, anayekipiga pale, West Bromwich Albion. **(Mail)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# HENRY SASA AFUNGUKA MAZITO ARSENAL IUZWE

Bado makubaliano hayajafikiwa, lakini sisi hapa ndio tumefika hadi kieleweke, ngoja tusubiri tuone...

**LONDON, England**

THIERRY Henry ameisisitizia Sky Sports, kwamba Daniel Ek amejiandaa kikamilifu kuinunua Arsenal, lakini familia ya Stan Kroenke bado haijajibu ofa yake.

Ek, ambaye alikuwa jukwaani kuishuhudia Arsenal ikiibuka na ushindi wa mabao 3-1, dhidi ya Tottenham Hotspur katika mchezo wa Ligi Kuu England, Jumapili, alimwandikia mmiliki Kroenke Mei mwaka huu kuwa tayari kutoa ofa ya pauni bilioni 1.8, ili kuinunua klabu hiyo ya London Kaskazini.

Lakini ofa hiyo hadi sasa bado ipo mezani kwa mmiliki huyo mfanyabishara raia wa Marekani.

Ek, ambaye ni mwanzilishi na mmiliki wa Kampuni ya Spotify anaimani kwamba, Kroenke ataisikiliza ofa hiyo - ambapo ataitoa yote na si kwa mafungu, huku akiungwa mkono na magwiji wa klabu hiyo, Henry, Patrick Vieira na Dennis Bergkamp.

Henry, ambaye alishinda mataji manne makubwa yakiwamo mawili ya Ligi Kuu England akiwa na klabu hiyo, amebainisha kwamba, hakuna mazungumzo yanayoendelea kwa sasa, lakini anaimani makubaliano yatafikiwa na familia hiyo ya Kroenke, itakubali kuiuza klabu hiyo.

"Ili kuweza kufikia mafanikio ya juu, unahitaji kuwa na mtu mwenye kuwajibika ipasavyo pembeni yako," alisema Henry, kwenye kipindi cha Monday Night Football cha Sky Sports.

"Bado makubaliano hayajifikiwa, lakini sisi na yeye (Ek) hapa ndo tumefika hadi kieleweke.

"Hivyo, ngoja tusubiri tuone nini kitatokea. Lakini kwa wakati huu, tunafurahia kwanza ushindi wa Jumapili.

"Ingawa bado hakuna mazungumzo yaliyofanyika kwa wakati huu, lakini nahisi yatafanyika wakati wowote na yatakuwa ya muda mrefu.

"Nilisema hapa mara ya mwisho wakati nikiwa kwenye kipindi hiki, Mei. Kwa muda gani hili jambo litafanyika, sijui kwa kweli."

Henry awali alinukuliwa akisema kwamba, Ek anataka kurudisha utambulisho wa Arsenal, uliopotea chini ya Kroenke.

Ek ni raia wa Sweden, ambaye ni shabiki wa Arsenal, tangu akiwa mtoto mdogo na amekuwa na nia ya dhati kutaka kuinunua klabu hiyo.

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 537

MECHI KALI
HOME
KAGERA SUGAR
4.85 | 3.10 | 1.77
YOUNG AFRICANS
AWAY

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa
halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# HAALAND APEWA NAFASI KUBWA KUTUA MADRID



**DORTMUND, Ujerumani**

MKURUGENZI wa Borussia Dortmund, Hans-Joachim Watzke, amekubali kwamba straika wake anayetakiwa sana, Erling Haaland ana nafasi kubwa zaidi ya kujiunga na Real Madrid.

Klabu nyingi zimekuwa zikimwania Haaland na kuna uwezekano akaondoka kipindi cha majira ya joto kinachokuja huku pia akiwa na kipengele cha kununuliwa cha pauni milioni 70.

Licha ya Real Madrid kuwania saini hiyo, lakini Manchester United nayo imekuwa ikihaha kuisaka saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21.

Hata hivyo, Real Madrid wana nafasi kubwa zaidi ya kumsajili Haaland pamoja na nyota Kylian Mbappe kutoka kule Paris Saint-Germain ambaye mkataba wake unamalizika mwakani.


Akizungumza na Sport1, Watzke amebainisha kwamba, Haaland ambaye ni raia wa Norway ana nafasi kubwa zaidi ya kujiunga na Real Madrid.

"Yeye ni mtu anayejitegemea," alisema Watzke akimzungumzia Haaland.

"Ninavyojua atakwenda kucheza katika moja ya klabu kubwa duniani, ingawa tayari anaicheza moja ya klabu kubwa duniani."

Kwa sasa mshambuliaji wa Manchester United, Anthony Martial anaonekana kuwa na nafasi kubwa zaidi ya kwenda kujiunga na Borussia Dortmund kama mrithi wa Haaland - kam

# Chelsea yajitosa kumsajili Chiesa



**LONDON, England**

CHELSEA inapanga kutoa ofa kwa ajili ya kumsajili nyota wa Juventus, Federico Chiesa katika miezi inayokuja.

Kocha Thomas Tuchel anaonekana kuwa shabiki wa Chiesa ili akaungane na Romelu Lukaku ambaye ametoka kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A.

Hata hivyo, ofa ya awali ya euro milioni 100 iliyoitoa Chelsea kipindi cha majira ya joto ilikataliwa na Juventus.

Lakini sasa Juve inaonekana kuwa tayari kumwachia Chiesa na mazungumzo yanaendelea kati ya Chelsea na Juventus kwa ajili ya kumchukua atue pale Stamford Bridge.

Licha ya mmiliki wa Chelsea, Roman Abramovich kuwekeza sana kwenye kikosi chake wakati wa dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto kilichopita, bado anataka kuendelea kuimarisha timu hiyo.

Kwa mujibu wa ripoti ya Daily Mail, Chelsea inaweza kumsajili Chiesa wakati wa kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

## HABARI MICHEZO

# 7,737,060 JACKPOT

## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 02.10.21 | 17:00 | Derby vs Swansea | 2.52 | 3.22 | 2.72 |
| 2. 02.10.21 | 17:00 | Peterborough vs Bristol City | 2.57 | 3.21 | 2.67 |
| 3. 02.10.21 | 17:00 | Luton Town vs Huddersfield | 2.39 | 3.25 | 2.86 |
| 4. 02.10.21 | 17:00 | Hull City vs Middlesbrough | 2.86 | 3.25 | 2.39 |
| 5. 02.10.21 | 17:00 | Blackpool vs Blackburn | 2.86 | 3.16 | 2.45 |
| 6. 02.10.21 | 17:00 | Barnsley vs Millwall | 2.27 | 3.20 | 3.11 |
| 7. 02.10.21 | 18:00 | Montpellier vs Strasbourg | 2.40 | 3.47 | 2.78 |
| 8. 02.10.21 | 19:30 | Brighton vs Arsenal | 2.85 | 3.15 | 2.58 |
| 9. 02.10.21 | 22:00 | Atletico Madrid vs Barcelona | 2.14 | 3.32 | 3.47 |
| 10. 03.10.21 | 16:00 | Tottenham vs Aston Villa | 2.14 | 3.46 | 3.36 |
| 11. 03.10.21 | 16:00 | Crystal Palace vs Leicester | 3.21 | 3.46 | 2.20 |
| 12. 03.10.21 | 18:00 | Lille vs Marseille | 2.45 | 3.29 | 2.84 |
| 13. 03.10.21 | 18:30 | Liverpool vs Manchester City | 2.75 | 3.39 | 2.52 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 29 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1077 | ECU Joondalup vs Adelaide Olympic | 2.04 | 4.05 | 2.80 |
| 13:00 | 5889 | Kawasaki Frontale vs Vissel Kobe | 1.49 | 4.27 | 5.24 |
| 14:00 | 5713 | Polisi Tanzania vs KMC | 2.32 | 2.81 | 3.25 |
| 15:00 | 4282 | Spartak II Moscow vs Tom Tomsk | 2.02 | 3.25 | 3.44 |
| 15:30 | 3997 | Junior Sevan vs Ararat Armenia | 5.03 | 3.39 | 1.66 |
| 16:00 | 4981 | Kagera Sugar vs Young Africans | 4.85 | 3.10 | 1.77 |
| 16:00 | 5147 | FC Krasnodar II vs FC Rotor Volgograd | 3.05 | 3.39 | 2.11 |
| 16:30 | 1491 | Olimpia Zambrow vs GKS Katowice | 7.93 | 5.22 | 1.29 |
| 16:30 | 3321 | Wieczysta Krakow vs Chrobry Glogow | 2.56 | 3.28 | 2.51 |
| 17:00 | 1313 | Benfica U19 vs Barcelona Youth | 2.71 | 3.44 | 2.30 |
| 17:00 | 1858 | Crewe U23 vs Wigan U23 | 2.03 | 3.53 | 3.14 |
| 17:00 | 3368 | KF Ballkani vs KF Feronikeli | 1.34 | 4.64 | 7.35 |
| 17:00 | 4258 | Strommen vs Kfum Oslo | 2.96 | 3.39 | 2.16 |
| 17:00 | 5741 | Grorud IL vs Ranheim | 4.07 | 4.07 | 1.66 |
| 17:30 | 3059 | Loko Tbilisi vs Dinamo Tbilisi | 3.19 | 3.24 | 2.12 |
| 18:00 | 2590 | Sokol Ostroda vs Pogon Siedlce | 5.82 | 4.17 | 1.46 |
| 18:00 | 3242 | Akron Tolyatti vs Yenisey Kr | 3.19 | 3.38 | 2.06 |
| 18:30 | 3305 | Urartu vs Artsakh | 2.25 | 3.25 | 3.25 |
| 18:40 | 4574 | Al Jabalain vs AL Adalh | 1.89 | 3.25 | 3.88 |
| 19:00 | 1474 | Torpedo Moscow vs Neftekhimik | 1.51 | 4.00 | 5.46 |
| 19:00 | 4700 | FC Elva vs Tallinna Kalev | 9.60 | 6.80 | 1.24 |
| 19:00 | 4871 | JK Welco Elekter vs FC Nomme United | 6.94 | 5.95 | 1.32 |
| 19:00 | 5847 | Aasane Fotball vs Sogndal | 3.44 | 3.54 | 1.92 |
| 19:30 | 4066 | Dila Gori vs Dinamo Batumi | 4.60 | 3.30 | 1.86 |
| 19:45 | 4768 | Zenit St Petersburg vs Malmo | 1.55 | 4.21 | 5.61 |
| 19:45 | 4893 | Atalanta vs BSC Young Boys | 1.44 | 4.90 | 6.20 |
| 20:00 | 2314 | Akropolis IF vs Jonkopings Sodra | 3.20 | 3.45 | 2.19 |
| 20:00 | 2528 | AL Khaleej Khor Fakkan vs Emirates Club | 1.48 | 4.36 | 5.23 |
| 20:00 | 3042 | Norrby IF vs Helsingborg | 2.54 | 3.13 | 2.88 |
| 20:00 | 3531 | Gais vs Orgryte IS | 2.71 | 3.11 | 2.71 |
| 20:00 | 4004 | GIF Sundsvall vs Trelleborgs FF | 2.55 | 3.35 | 2.70 |
| 20:00 | 5594 | Stabaek vs Stromsgodset | 2.72 | 3.56 | 2.35 |
| 20:00 | 5975 | Falkenbergs vs Landskrona Bois | 2.15 | 3.34 | 3.39 |
| 20:45 | 3267 | Stomil Olsztyn vs Sandecja | 2.84 | 3.18 | 2.33 |
| 21:05 | 3598 | Raith Rovers vs Dunfermline | 2.03 | 3.33 | 3.43 |
| 21:15 | 1157 | Difaa El Jadidi vs FAR Rabat | 2.43 | 3.06 | 2.81 |
| 21:45 | 1273 | Millwall vs Bristol City | 2.04 | 3.11 | 3.80 |
| 21:45 | 2288 | Luton Town vs Coventry | 2.67 | 3.07 | 2.67 |
| 21:45 | 2833 | Derby vs Reading | 2.27 | 3.11 | 3.20 |
| 21:45 | 3069 | Barnsley vs Nottingham | 2.43 | 2.90 | 3.14 |
| 21:45 | 5027 | Cray Wanderers vs Wingate and Finchley | 1.85 | 3.73 | 3.49 |
| 21:45 | 5036 | Fulham vs Swansea | 1.37 | 4.75 | 7.32 |
| 21:45 | 5308 | Peterborough vs Bournemouth | 4.75 | 3.61 | 1.70 |
| 22:00 | 1666 | Benfica vs Barcelona | 2.75 | 3.33 | 2.53 |
| 22:00 | 1691 | Santiago Wanderers vs Univ de Chile | 3.59 | 3.20 | 1.99 |
| 22:00 | 2839 | Bayern Munchen vs Dynamo Kiev | 1.08 | 10.98 | 23.97 |
| 22:00 | 3339 | RB Salzburg vs Lille | 1.98 | 3.56 | 3.66 |
| 22:00 | 3357 | Manchester Utd vs Villarreal | 1.58 | 4.18 | 5.32 |
| 22:00 | 5412 | VfL Wolfsburg vs Sevilla FC | 2.90 | 3.20 | 2.49 |
| 22:00 | 5884 | Juventus vs Chelsea | 4.10 | 3.45 | 1.90 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# RAMSEY KUWEKWA SOKONI JUVE JANUARI




**TURIN, Italia**

KLABU ya Juventus ya Italia inajipanga kumweka sokoni kiungo wake kutoka nchini Wales, Aaron Ramsey katika dirisha lijalo la usajili la majira ya baridi, Januari.

Nyota huyo wa zamani wa Arsenal, amepoteza namba katika kikosi cha kwanza cha wababe hao wa Turin.

Taarifa hiyo imezifungua macho timu za West Ham, Everton na Newcastle United ambazo zimeanza kuulizia uwezekano wa kuipata huduma ya kiungo huyo ambaye mkataba wake na Juventus utafikia kikomo mwaka 2023.

Ramsey mwenye umri wa miaka 30, amekuwa akipambana kuingia katika kikosi cha kwanza cha Juventus ambayo imepanga kuachana naye katika dirisha lijalo kama mchezaji huru.

Nyota huyo ni miongoni mwa wachezaji wanaopokea mshahara mkubwa katika Ligi Kuu Italia, Serie A, jambo ambalo linazipa ugumu timu nyingi zinazohitaji huduma yake.

Kiungo huyo anajua kila kitu kuhusu Ligi Kuu England baada ya kucheza kwa miaka 11 akiwa katika kikosi cha 'Washikabunduki' hao wa London ambao walimwamini tangu akiwa kinda.

Nyota huyo alijiunga na Arsenal mwaka 2008 akitokea Cardiff City baada ya kukosa nafasi alitolewa kwa mkopo kwenda Nottingham Forest, baadaye alirejea na kuwa miongoni mwa wachezaji tegemeo katika kikosi cha Arsene Wenger.

Katika miaka 11 aliyokaa Arsenal, nyota huyo ana rekodi ya kuvutia baada ya kucheza michezo 371, akifunga mabao 65 na kutoa pasi za mabao 65 katika mashindano yote aliyocheza.

Katika kipindi chote alichodumu Arsenal, alifanikiwa kushinda mataji matatu ya FA pamoja na Ngao za Jamii mbili, lakini alitimka mitaa ya Colney mwaka 2019 na kujiunga na 'Kibibi Kizee' hicho cha Turin kama mchezaji huru.



# Neville: United haina nafasi ubingwa EPL

**MANCHSTER, England**

MANCHESTER United, hawana ubavu wa kutwaa taji la Ligi Kuu England (EPL), msimu huu kwani taji hilo lipo mikononi mwa Manchester City, kwa mujibu wa Gary Neville.

Neville ameweka wazi matumaini kwa timu hiyo kuweza kutwaa taji hilo kubwa kwa sasa ni madogo hasa kutokana na ubora wa wapinzani wao, huku United wakicheza bila kushirikiana.

Pia ameshauri kwamba kwa sasa ni muhimu kwa Man United kumweka kando kocha wao Ole Gunnar Solkajaer na kumpa mikoba Antonio Conte kwa kuwa wengi hawamwelewi kocha huyo jambo analolitafuta ndani ya ligi.

Haya yote yamekuja kutokana na mwendo wa kinyonga wa Man United kwenye kusaka matokeo ambapo ilipoteza kwa kufungwa mabao 2-1 kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya mbele ya Young Boys, kisha ikanyooshwa na West Ham United na Aston Villa kote iliambulia bao mojamoja, kwenye mechi hizo za Ligi Kuu England.

Leo, Septemba 29 United ina kibarua cha kusaka ushindi mbele ya Villarreal katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na haipewi nafasi ya kushinda kutokana na kushindwa kutabirika licha ya uwapo wa nyota mkubwa Cristiano Ronaldo ndani ya kikosi hicho.

"Nafikiri hivi hata pale wanaposhinda na hata Ronaldo anapofunga bado wamekuwa hawachezi vizuri kama timu kwa kushirikiana.

# Michezo

Jumatano Septemba 29, 2021

Nipashe




**Henry sasa afunguka mazito Arsenal iuzwe** UKURASA 21

KIMBIZA...



Winga wa Simba, Hassan Dilunga, akimtoka mchezaji wa Biashara United huku mshambuliaji Meddie Kagere akifungua chumba tayari kwa kupokea pasi, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume mjini Musoma jana na kumalizika kwa sare tasa. **PICHA: SIMBA**

# SIMBA YASHIKWA SHARUBU MUSOMA

## ●●● Bocco ashindwa kulinda rekodi zao Karume, Dodoma Jiji, Mbeya City zaifuata Namungo kileleni, huku...

**Na Adam Fungamwango**

HUKU wakikosa mkwaju wa penalti dakika ya pili ya nyongeza, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, jana walilazimishwa sare ya bila kufungana na Biashara United kwenye Uwanja wa Karume mjini Musoma.

Ilikuwa nafasi pekee ya Simba kujipatia pointi tatu kwenye mechi ya kwanza ya Ligi Kuu, lakini kipa Mganda, James Ssetuba, alipangua penalti ya nahodha John Bocco, iliyotokana na Pape Sakho aliyeingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Meddie Kagere kuangushwa ndani ya eneo la hatari.

Hii ni mara ya kwanza kwa Simba kutoshinda kwenye uwanja wa huo tangu Biashara United ipande daraja na kuanza kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara.

Msimu wa kwanza 2018/19, Simba ilishinda mabao 2-0, msimu wa 2019/20 ikapata tena ushindi kama huo huku msimu uliopita ikishinda bao 1-0.

Mechi ilianza kwa butuabutua kwa pande zote mbili, huku Biashara United wakiongeza na matumizi ya nguvu, hali iliyosababisha mashabiki kutoshuhudia kandanda safi.

Hii ilitokana na hali ya uwanja kutoruhusu pasi za chini, hata hivyo ilichukua dakika 20 ndipo shambulizi la hatari lilipotokea kwa Kagere ambaye alianza jana, alipounganisha mpira wa krosi uliopigwa na Rally Bwalya, lakini ukatoka nje kidogo ya lango la Biashara United.

Mnyarwanda huyo pia alipiga shuti la mguu wa kushoto dakika ya 33, lakini liliendа nje kutokana na kuzongwa na mabeki wa Biashara United, hivyo kutompa nafasi ya kupiga vizuri.

Sekunde chache baadaye, mchezaji chipukizi wa Biashara United, Denis Nkane nusura aipatie timu yake bao baada ya kuwatoka mabeki wa Simba na kuwahi pasi ya juu iliyotolewa na Ramadhani Chombo 'Redondo', akiwa anatazamana na Aishi Manula, lakini kwa mastaajabu ya wengi, akapaisha mpira juu.

Simba ilinusurika tena kufungwa dakika tano kabla ya kwenda mapumziko, baada ya mabeki wa timu hiyo kuzembea kuokoa hatari na kuzua kizaazaa, ambacho kiliamualiwa na Manula aliyekuwa ametoka golini, lakini alirerejea tena langoni kuudaka mpira uliokuwa ukigombewa na wachezaji wa timu zote mbili.

Kipindi cha pili timu zote zilifanya mabadiliko, lakini Simba ilinufaika zaidi na mabadiliko ya kuwatoa Shomari Kapombe, Hassan Dilunga, Kagere, Henock Inonga, na Bwalya, ikiwaingiza Duncun Nyoni, Mohamed Hussein, Peter Banda, Yusuph Mhilu na Pape Sakho, ambao kwa kiasi kikubwa waliifanya timu hiyo kushambulia zaidi, huku wapinzani wao wakifanya kazi ya kuokoa kwa kupiga mbele.

Nafasi hatari zaidi kipindi cha pili zilikuwa dakika ya 68, wakati Erasto Nyoni alipopiga shuti lililopaa juu kidogo ya lango baada ya kuanzisha faulo haraka, Peter Banda na Sakho nao walifanya mashambulizi makali mwishoni mwa mchezo, huku Salum Kipaga wa Biashara United akipiga faulo maridadi ambayo kama si uhodari wa kipa Manula, ingeweza kujaa wavuni.

Katika mechi nyingine zilizopigwa jana Mbeya City iliichapa Tanzania Prisons kwa bao 1-0 katika Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya huku Dimba la Jamhuri jijini Dodoma, Dodoma Jiji FC nayo ikipata ushindi kama huo dhidi ya Ruvu Shooting.

Kwa matokeo hayo, Namungo FC inaendelea kutesa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi tatu sawa na Mbeya Kwanza FC, Dodoma Jiji na Mbeya City, lakini ikishika nafasi hiyo ya juu kutokana na idadi kubwa ya mabao.

## Yanga, Kagera Sugar ni vita leo

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Yanga ikianza mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Bara leo, Kocha Mkuu wa miamba hiyo ya mtaa wa Twiga na Jangwani jijini Dar es Salaam, Nasreddine Nabi, amesema anatambua hautakuwa mchezo rahisi, lakini wamejipanga kuhakikisha wanaanza vizuri msimu huu wa 2021/22.

Yanga ambayo itashuka katika Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba leo kuwavaa wenyeji wao, Kagera Sugar, itakuwa na ari kubwa ya kuendelea kupata matokeo baada ya kuwalamba watani zao, Simba bao 1-0 na kutwaa Ngao ya Jamii Jumamosi iliyopita kwenye Dimba la Benjamin Mkapa.

Akizungumzia mchezo huo, Nabi alisema kikosi chake kipo tayari na anatambua mchezo huo utakuwa mgumu, lakini kama wachezaji wake watatekeleza yale aliyowaelekeza mazoezini, hana shaka katika kupata matokeo.

Alisema anatambua Kagera Sugar pia itakuwa imejipanga kupata matokeo hasa ukizingatia itakuwa nyumbani, lakini malengo yake ni kuhakikisha wanaanza vizuri msimu ili kutekeleza malengo yao mwishoni mwa msimu.

"Hautakuwa mchezo rahisi hasa kwa kuzingatia Kagera Sugar watakuwa nyumbani, lakini hiyo haiwezi kuwa sababu kwetu kushindwa kupambana kupata matokeo," alisema Nabi.

Kocha wa Kagera Sugar, Francis Baraza, alisema pamoja na kwamba Yanga ni klabu kubwa, wataiheshimu kwa hilo lakini hawana sababu yoyote ya kuiogopa.

"Bado ninaendelea kuwaweka sawa wachezaji wangu kutafuta kombinesheni nzuri, ninauhakika utakuwa msimu mgumu ikiwa ni pamoja na mchezo huu dhidi ya Yanga," alisema.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >